ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaybah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nne – Tarehe 16 Juni, 2010

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 49

Maafa ya Mvua za Masika

Mhe. Ali Abdulla Ali –Aliuliza:-

Mhe. Spika, katika mvua za masika zilizonyesha nchini, maeneo mbali mbali yakiwemo Kilombero, Bumbwini, Kihinani na baadhi ya maeneo ya mjini watu wamepata maafa ya mafuriko na baadhi ya nyumba kuanguka.

(a) Je, Mhe. Waziri, Serikali imetoa msaada gani kwa watu waliothiriwa na mvua hizo?

(b) Kama umetolewa msaada, kiasi gani cha fedha kimetumika kwa msaada huo?

(c) Kwakuwa kila mwaka kuna msimu wa mvua za masika ambazo mara nyingi huleta madhara katika baadhi ya maeneo Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na maafa ya aina hiyo?

Mhe Waziri Kiongozi - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo;-

Mhe. Spika ni kweli kwamba katika msimu huu wa mvua wakaazi wengi wa maeneo mbali mbali mjini na vijini waliathirika kutokana na mvua hizo. Hata hivyo, kwa ushirikano wa Mamlaka ya Hali ya Hewa kanda ya Zanzibar hali ya kuwepo kwa hali hiyo ilitangazwa mapema na kuwataka wananchi wachukue hadhari kutokana na hali hii.

Aidha, naomba kutoa ufafanuzi kuwa, sheria ya kukabiliana na maafa ya mwaka 2003, imefafanua vizuri muundo wa kamati za kukabiliana na maafa

hapa Zanzibar na pia majukumu katika kila kamati. Moja wapo ya majukumu hayo ni kuzitaka kamati za maafa za Wilaya na Mikoa kushughulikia maafa katika maeneo yao, ambapo kama kamati hizo zitashindwa zinatakiwa kuwasilisha matatizo hayo katika Mikoa na Mkoa ukishindwa ndio utawasilisha katika vyombo vya juu ikiwemo Afisi ya Waziri Kiongozi.

a). Mhe. Spika katika eneo la Mkoa Mjini, Magharibi wizara ilipokea taarifa kutoka katika Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Mkoa juu ya kuwepo mwananchi katika eneo la Mpendae ambaye nyumba yake ilijaa maji kabisa. Ofisi yangu kwa kushirikiana na kamati hiyo pamoja na Mbunge na Mwakilishi katika eneo hilo waliweza kutoa msaada wa dharura kwa mwananchi huyo ambaye kwa kipindi hicho alihifadhiwa na jirani yake. Aidha, katika maeneo yaliyo mengi hadi hivi sasa serikali kuu haijapokea rasmi taarifa kuhusu maafa yaliyotokea katika sehemu hizo zilizotajwa huko juu; na

b). Gharama zilizotumika kwa ajili ya kumsaidia mwananchi huyo inakadiriwa ni shilingi 100,000/= zilizotumika kwa ununuzi wa gorodo na mablangeti.

c) Mhe. Spika kutokana na hali hii serikali inaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- Kuendelea kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa katika kutoa taarifa na tahadhari za mapema kwa wananchi kuhusiana na mwenendo mzima wa mvua;

- Kutoa taaluma kwa jamii, juu ya kujikinga na maafa ya aina mbali mbali zikiwemo mvua;

- Kuendelea kuelimisha jamii kutojenga katika maeneo holela hasa katika maeneo ya mijini;

- Kuacha tabia ya kutia taka katika mitaro ya kupitishia maji, hali ambayo kwa kiasi kikubwa inachangia katika kusababisha mafuriko katika maeneo ya mjini;

- Kuhakikisha taasisi husika za serikali zinatimiza majukumu yao yakiwemo ya kufanya usafi kwa Baraza la Manispaa pamoja na kudhibiti ujenzi holela kwa mamlaka za ardhi; na

- Idara ya kukabiliana na maafa kwa kushirikiana na *UNICEF* imechukua hatua za kujiandaa kwa kuweka ghala liliopo eneo la

Saateni kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vya misaada ya kiutu na vya kibinadamu vitakavyoweza kutumika wakati wa dharura.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Waziri Kiongozi swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, hivi karibuni katika hizi za Masika zinazoendelea katika Jimbo la Micheweni kumeshatokea maafa mara mbili. Mara ya kwanza kulitokea maafa ya kuanguka jiwe likawaelemea watu na wakafa watu wawili. Pia juzi katika mvua hizi zinazoendelea lilianguka jiwe likawaelemea vijana watatu wa, mmoja mwanafunzi wa skuli akapoteza maisha yake.

Je, Mhe. Waziri suala hili analijua na kama analijua je, wananchi wale waliopata maafa hayo serikali inawaangalia vipi kuwasaidia wananchi hao?

Mhe Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama nilivyosema awali ni jukumu la serikali kuwasaidia wananchi wake wanaopata maafa katika maeneo mbali mbali hapa Zanzibar. Lakini jukumu la awali kwa kuwa kuna kamati mbali mbali za Wilaya kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, katika maeneo mbali mbali Wilaya na Mikoa zipo kamati za kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, jukumu la Afisi ya Waziri Kiongozi ni kupokea taarifa mbali mbali. Kwa hivyo, nakubaliana naye kama kulikuwa na tatizo kama hilo kama mtu mmoja alifariki kwa kuangukiwa na jiwe, pia kuna mwanafunzi nae amefariki.

Mhe. Spika, taarifa hizi bado sijazipokea katika Afisi yangu ya Waziri Kiongozi, lakini kwa kuwa taarifa hizi tumezipokea katika Baraza lako tukufu ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba baada ya kumaliza tu kikao hiki nitajaribu kuitafuta taarifa hii na hatua tutakayofikia nitajaribu kumuarifu hata katika kipindi cha jioni ili afisi yangu iweze kuchukua hatua zinazopaswa haraka iwezekanavyo ili tumsaidie mwananchi huyo ambaye anastahiki kusaidiwa na serikali yake.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri Kiongozi swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni nini madhumuni ya Kamati ya Maafa.

Na je, kamati hii inapotoa misaada miezi mitatu baada ya maafa kutokea lile suala zima la kusaidia wanaopata maafa linafikiwa.

Mhe Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, madhumuni ya Kamati za Maafa kwanza ni kutathmini hali ya maafa, kutabiri hali ambayo inaweza kutokezea wakati kutakapotokea hali ya mabadiliko ya hali ya hewa na kadhalika. Sasa jukumu

lake mara nyingi ni kunapotokea maafa kazi yake kuu ni kufuatilia hayo maafa wenyewe kuangalia ni watu gani ambao wameathirika na kwa kiasi gani wameathirika na mchango gani unatakiwa kutolewa na serikali.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mara nyingi yanapotokea maafa ni lazima chombo kinachohusika Kamati za Maafa za Wilaya au Afisi ya Waziri Kiongozi ni lazima iende iangalie hiyo hali iliyotokea, ifanyiwe tathmini na tujue kwa kiasi gani jambo lipi linafanywa na serikali. Mhe. Spika, baada ya hapo baada ya kujua ni lazima sasa serikali itafute uwezo huo kama fedha ziko tayari tunawalipa, lakini kama fedha haziko tayari katika Afisi ya Waziri Kiongozi tunachotakiwa kukifanya ni kuomba serikalini ili tumlipe mwananchi huyo.

Mhe. Spika, kwa ujumla hatua hizo zinaweza zikachukua muda wa mwezi mmoja, wakati mwengine zinaweza kuchukua hata muda wa miezi miwili, lakini inategemea sana taarifa zile za awali kutoka katika Wilaya na Mikoa. Mhe. Spika, taarifa hizi zikifanyiwa kwa haraka na tutajaribu kufanya kila tulilonalo katika uwezo wetu kuwahimiza wenzetu kamati hizi za maafa katika Wilaya wahakikishe kwamba kazi hiyo ya kutathmini inafanywa haraka iwezekavyo. Kwa sababu ikifanywa haraka iwezekanavyo na ikifanywa mapema na Afisi ya Waziri Kiongozi ikapata taarifa hizo na sisi tutakuwa tunaomba fedha serikali mapema iwezekanavyo.

Kwa hivyo, naomba nimuhakikishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba nakubaliana nae kuwa sio busara mwananchi ambaye amepata maafa kuchukua muda mrefu anatakiwa kulipwa angalau kumfuta jasho. Mhe. Spika, namuhakikishia mheshimiwa kama nilivyosema tutashirikiana na kamati hizi za Wilaya ili kazi hii ya kufanya tathmini ifanyike mapema ili na sisi tuweze kufanya utaratibu wa kumlipa mwananchi huyu mapema iwezekanavyo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimechanganyikiwa kujua nini maafa na ajali, maana yake maafa yanavigezo vyake na ajali ina vigezo vyake. Mhe. Spika, pale mjumbe anaposema kwamba kuna mtu ameangukiwa na jiwe mimi najua ni ajali, na maafa vigezo vyake ni lile janga ambalo ni kubwa mpaka mataifa yanajua na kuna michango ya kimataifa. Lakini pamoja na hayo hivyo nauliza kama Zanzibar ni nchi na imo katika dunia na ina haki ya kupata misaada ya maafa kutoka huko ulimwenguni.

Je, serikali yetu mfuko wake una kiasi gani cha maafa ili kupunguza hayo matatizo yanapotokea na wananchi waridhike.

Mhe Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Mwakilishi kwa maelezo yake ya utangulizi, ufafanuzi mzuri alioutoa tofauti ya kati ya ajali na maafa. Mhe. Spika, hilo nakubaliana naye na ndio hatua ambayo mara nyingi tunayoichukua, mara nyingi yanapotokea maafa hasa katika yale masuala ambayo hatuna uwezo wa kukabiliana nao tumekuwa tukiwasiliana na taasisi mbali mbali za kikanda na kimataifa ili kuweza kupata misaada mbali mbali.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la Mfuko wa Maafa katika Afisi ya Waziri Kiongozi hivi sasa una kiasi gani katika kukabiliana na maafa. Nafikiri Mhe. Mwakilishi atakakubaliana na mimi kwamba katika bajeti iliyopita ya mwaka 2009-2010 hakukuwa na kifungu maalum kilichotengwa kwa ajili ya mfuko wa maafa. Fedha ambazo zimetengwa mwaka jana zilikuwa ni kwa ajili ya kushughulikia shughuli mbali mbali za uendeshaji wa Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, nakumbuka Waheshimiwa Wajumbe wakati wa kupitisha vifungu katika Afisi ya Waziri Kiongozi walikuwa wakali sana katika suala hilo. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Mwakilishi ni kwamba mara nyingi yanapotokezea matatizo mbali mbali yanayohusiana na maafa hakuna kifungu ambacho tayari kimetengwa, mara nyingi tunategemea hazina moja kwa moja inapotokea maafa kama nilivyosema wakati nilipokuwa nikimjibu Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwamba mara nyingi yanapotokea maafa tunafanya tathmini. Kwa hivyo, kama Afisi ya Waziri Kiongozi inazo fedha za kulipa kwa ajili ya mwananchi ambaye amepatwa na maafa tunafanya hivyo, kama haina fedha za kutosha basi tunawasiliana na Wizara ya Fedha moja kwa moja ili waweze kutupatia fedha hizo kutoka mfuko mkuu wa serikali, ndio utaratibu ambao tumekuwa tukiufanya katika kipindi hiki cha mwaka mmoja uliopita.

Nam. 24
Kituo Cha Gari za Abiria Chake Chake

Mhe. Said Khelef Ali (Kny: Mhe. Haji Mkema Haji) - Aliuliza:-

Katika Mji wa Chake-Chake hakuna kituo maalum cha magari ambacho abiria wanapata huduma za usafiri kwa utulivu.

(a) Kwa nini Baraza la Mji Chake-Chake Serikali halijajenga?

(b) Kwa sasa huduma za kupakia na kushusha abiria na mizigo zinafanyika njiani, karibu na jengo la zamani la Chake Chake Hotel ambalo sasa ni Tawi la *BARCLAYS BANK*. Mhe. Waziri, huoni kuwa hilo ni jambo la hatari kwa usalama wa wapita njia na usalama wa huduma za benki hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 24 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kwa sasa Mji wa Chake Chake hauna kituo maalum cha magari ya abiria ambacho wananchi wanapata huduma kwa utulivu baada ya kituo cha zamani kiliopo Marikiti kuvamiwa na wafanya biashara. Hata hivyo, Serikali kupitia Baraza la Mji Chake lina mpango wa kujenga kituo kipya cha magari ya abiria katika eneo la mava ya Mbarouk jirani na Michakaini. Kuanza kwa kazi hiyo kunategemea kupatikana kwa fedha jumla ya Tshs. Bilioni 1.2 zikiwa ni pamoja na Tshs. Milioni 14 za kulipia fidia.

Mhe. Spika, kwa taarifa ambayo nimeipata tena kati ya jana na leo ni kwamba baadhi ya fidia zimeshaanza kulipwa kwa wananchi na wanaendelea kutayarisha mipango iendelee vizuri. Kwa hivyo, maandalizi kwa ujumla yanaendelea vizuri kwa mashirikiano kati ya Madiwani na Katibu wa Baraza la Mji. Kwa hivyo, wakati najibu suala hili ilikuwa fidia walikuwa hawajaanza kupewa, lakini sasa hivi zimeshaanza kutolewa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mara nyingi wakitoka huko vijijini wakipanda magari ya abiria huwa wanafuatia maeneo ya mjini na hasa sokoni kwa ajili ya mahitaji yao. Lakini eneo alilolitaja hapa kuwa litajengwa kituo cha daladala liko mbali sana na mji, haoni kama kufanya hivyo bado hajawaondoshea wananchi udhia wa kufika kwenye mahitaji yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ: Mhe. Spika, ukweli katika suala la biashara wananchi hufuata biashara, biashara huwa haifuati wananchi. Hata ukichukua mfano wa sasa hivi hapa Darajani wameondoshwa dada njoo wamekwenda Saateni na wananchi wamewafata kule kule Saateni. Kwa hivyo, katika suala zima la biashara mara nyingi wananchi hufuata kule ambako biashara hiyo inafanyika. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi kwa suala hili ni hatua nzuri kwani tunajaribu kuweka mazingira mazuri ili shida hizo ambazo ulizofikiria zisiwepo.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anasema kwamba kunataka kujengwa sehemu mpya ya magari katika Mava ya Mbarouk, sisi tulioko Pemba mava hiyo tunaijua ni kwamba pale pana bonde kubwa sana

ni uwanda gani pale atakapotujengea sehemu ya kuweka magari na ikawezekana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ: Mhe. Spika, kwanza nakiri kwamba kwenye eneo hilo mimi sijafika. Lakini kwa kufuatilia utendaji na malipo ni kwamba sehemu hiyo ndio iliyoteuliwa kujenga. Hata hivyo, Mhe. Mwakilishi nitaomba ushirikiano wako tutakapomaliza Baraza hili kwenda kukagua kwa suala zima la *stand* hiyo.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza. Mhe. Spika, kutoka Mava ya Mbarouk mpaka Mjini Chake-Chake ni kilomita zisizopungua mbili na kidogo. Je, ukitilia maanani kwamba hapa hapana hata jengo moja la biashara anakusudia nini waziri ni kusema kwamba watu wakishakuteremka mava ya Mbarouk wende kwa miguu mpaka Chake Chake Mjini kutafuta shughuli za biashara.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ: Mhe. Spika, kama nilivyokwishakusema wakati namjibu Mhe. Raya ni kwamba naomba na wewe mheshimiwa suala hili tushirikiane pamoja ili tuangalie sehemu gani itakuwa ni nzuri kwa kazi hii.

Nam. 19

Shamba la Makurunge - Bagamoyo

Mjumbe aliyeuliza swali hili amelifuta.

Nam. 5

Kozi ya Vector Control

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Hivi sasa wako wafanyakazi saba ambao wanasoma kozi ya *Vector Control* katika kituo cha mafunzo cha *Vector Control Training Centre*, Tanga. Lakini wanne wanalipiwa na Serikali kupitia ufadhili wa *ADB* na watatu wanajitegemea.

(a) Mhe. Waziri, kwa wafanyakazi hao wote walituma maombi yao wakati mmoja, kwa nini walipewa nafasi za ufadhili baadhi tu na wengine wakakoseshwa.

(b) Kwa kuwa lengo ni kuwa na wataalamu wengi wa fani hiyo kwa ajili ya kukidhi mahitaji yaliyopo, kwa nini Serikali isiwalipie wafanyakazi waliobaki ili kuwatia moyo.

(c) Je, ni kweli kwamba katika utoaji wa nafasi za masomo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutenga nafasi kwa mgawanyo wa Unguja na Pemba. Kama ni kweli kwa nini iwe hivyo wakati mkataba wa kazi unamtaka mfanyakazi kufanyakazi popote ndani ya visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 5 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kuna wafanyakazi saba masomoni Mkoani Tanga katika fani ya *Vector Control* ambapo wafanyakazi wane wanalipiwa kwa ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB).*

Mhe. Spika, napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kuwa *ADB* inaendelea na mpango wa kulipia mafunzo ya kada mbali mbali kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kipindi cha miaka mitano (2007 – 2012) katika mpango huo huwa kuna idadi maalum ya wanaolipwa kwa kila mwaka. Kwa kozi ya *Vector Control ADB* ilipanga kuwalipia wafanyakazi watatu tu, lakini waliofaulu kujiunga na mafunzo kwa mwaka 2009 walikuwa saba.

Mhe. Spika, hata hivyo *ADB* ilimudu kuwalipia wafanyakazi wanne badala ya watatu kama ilivyopanga awali, wafanyakazi watatu walibakia wameingizwa katika orodha pamoja na wengine wakati wizara ikiendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka Serikalini na kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kugharamia mafunzo hayo.

Mhe. Spika, kwa muktadha wa suala hili hakuna mgawanyo wala upendeleo katika utoaji wa nafasi za masomo kwa Unguja na Pemba bali kila anaestahiki na akafuata utaratibu hupatiwa nafasi na ufadhili kama inavyostahiki bila ya ubaguzi wa aina yeyote.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amesema kwamba ADB ilikuwa na uwezo wa kuwafadhili wafanyakazi 4 na watatu wanajisomesha kwa mfuko wao wenyewe. Na kwa kuwa wizara inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kozi kama hizo.

a) Je, pale ambapo fedha itapatikana wizara itakuwa tayari kuwarejeshea fedha zao wale ambao wanajihudumia wenyewe?

b) Amesema kwamba hakuna utaratibu wa kutoa nafasi za masomo kwa upendeleo. Lakini mkataba wa kazi unaonesha kwamba mfanyakazi anaweza akafanya kazi Zanzibar au Pemba kwa nini nafasi hizi mkazigawa Pemba zake na Unguja zake?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nieleze kidogo kuhusu haya mafunzo tunayoyatoa. Ni kwamba kuna mkataba maalum wa *ADB* una *document* ya mafunzo tuliyokubaliana Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na *ADB*. Tukija kwenye sehemu ya *vector control* kwanza nini *vector control. Vector control* ni kupiga vita wale wadudu wanaoambukiza maradhi kama mbu, analeta maradhi ya malaria na vidudu vyenginenyo. Kwa hivyo, vile vidudu ndivyo tunavyovipiga vita.

Kwa hivyo, tulikubaliana na *ADB* kila wilaya asomeshwe mtu mmoja mmoja Unguja na Pemba katika *document* ile. Sasa mwaka 2008 tulikubaliana kupeleka wanafunzi watatu Tanga, wanafunzi waliopelekwa wametoka Micheweni, Ndugu Badru, Mjini Unguja Ndugu Mwanajuma na Chake Chake, Ndugu Ali Khamis. Mwaka 2009 tulipeleka kutoka Wete Bi Shadya, Mkoani ndugu Yahya na Magharibi, ndugu Makame na Kaskazini 'A' ndugu Mosi Kali.

Sasa nafasi zilizosalia ni tatu kwa mkataba na *ADB*. Tunazo nafasi hizo mpaka mwaka 2012, bado Kaskazini 'B', Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini. Walioko Tanga hivi sasa wale watatu wanatoka Pemba na *ADB* wanaesema Wilaya za Pemba zimekwishakamilika. Kwa hivyo, tunajitahidi kuwatafutia wafadhili wengine aidha kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au sehemu nyengine kwa sababu wale ni wafanyakazi wetu.

Sasa tutapofaulu kuwapatia watu wa kuweza kuwalipia naona wizara hatutokuwa na uwezo wa kuwalipa gharama waliyokwishajilipia. Kwa hivyo, watatustahamilia, huku tunakwenda mbio tukipata wafadhili tutawasaidia na hao watatu, kwa sababu ni wafanyakazi wetu.

Swali la pili sikulipata vizuri Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Hija Hassan Hija hebu rudia swali la pili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kimsingi swali langu la pili amelijibu. Kwa sababu nilikuwa nikitaka kujua kwamba mkataba wa kazi hausemi kuwa huyu aende Pemba huyu Unguja. Lakini amechanganya nimeridhika.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kasema kuwa wizara imo katika kutafuta mfadhili wa kuwalipia hawa watatu wengine waliobaki, na kwa kuwa kuna uwezekano ama wa kupata au kukosa mfadhili, endapo akakosekana mfadhili na wafanyakazi wale wakajihudumia wenyewe mpaka wakamaliza.

(a) Watakaporudi watafanyiwa maarifa ya kulipwa pesa zao walizotumia katika masomo.

(b) Ikiwa haitakuwa hivyo. Je, watakuwa na haki ya kujitafutia wenyewe pahali pa kufanya kazi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, hawa ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wanapata mshahara wao kama kawaida na mambo yao yote ya stahiki za Wizara ya Afya. Watapomaliza masomo tutawapokea, tutawapangia kazi za *Vector Control* katika wilaya zao.

Sasa taaluma siku zote mtu anaitafuta Mhe. Spika, na wala wizara yetu hatuzuwii watu wasijiendeleze. Mtu akipata nafasi akituomba ruhusa ni muhimu tu, aseme ninao uwezo au ninae mtu wa kunisaidia sisi tunamruhusu. Lakini narejea tena, tutaendelea kwa kadiri ya uwezo wetu kuwatafutia wafadhili na tukipata *Inshaallah* tutawalipia. Lakini kuwalipa gharama hizo siwezi kutoa ahadi hiyo Mhe. Spika.

Nam. 39

Mradi wa Maji Safi Mfenesini, Bumbwini na Kitope

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Tunaishukuru serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa mradi mkubwa wa maji safi na salama katika majimbo ya Mfenesini, Bumbwini na Kitope. Mradi huo sasa umeanza utekelezaji ambapo visima vitatu vimechimbwa eneo la Mfenesini na tangi limejengwa na ulazaji wa mabomba katika maeneo husika unaendelea.

(a) Je, Mhe. Waziri mradi huu umefadhiliwa na taasisi gani na una gharama ya kiasi gani cha fedha?

(b) Hivi sasa kunaundwa kamati katika shehia kusimamia mradi huo utekelezaji wake. Je, fedha za kuhudumia kazi za kamati hiyo zitatoka wapi?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika , kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 39 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo :-

Mhe Spika, Mradi wa Maji wa Mfenesini, Bumbwini ni miongoni mwa miradi yenye lengo la kuwaondoshea kero wakaazi wa Shehia 18 pamoja na maeneo ya jirani. Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili kwa pamoja baina ya Jumuia ya Ulaya (*European Union*) na Jumuia isiyo ya serikali ya Italy (*ACRA*).

Mhe. Spika mradi unategemea kutumia jumla ya Euro 1,049,000 ambazo ni sawa na shilingi 1,888,200,000/= za Kitanzania, ambapo kati ya fedha hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechangia jumla ya Euro 149,000 sawa na shilingi 268,200,000/= Jumuiya ya Ulaya, Euro 750,000 sawa na shilingi 1,350,000,000/= na *ACRA* ni Euro 150,000 sawa na shilingi 270,000,000/=.

Mhe. Spika ni kweli Mradi wa Maji Mfenesini, Bumbwini unategemewa kuendeshwa kwa usimamizi wa Kamati za Shehia ambapo hatua ya awali ilikuwa ni kuundwa kwa kanuni za uendeshaji wake ikiwa ni pamoja na maelezo ya jinsi kamati zitakavyopata mapato ya uendeshaji. Hata hivyo, kwa kumtoa wasi wasi Mhe. Mwakilishi, kamati zinategemewa kuendeshwa kwa michango ya maji itakayopatikana katika mifereji ya nje (*water kiosk*) itayowekwa katika maeneo husika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kamati zinazoshughulikia mradi wa maji kwa kuuendeleza watakuwa wanalipwa kutokana na *fund* itayokusanywa na mifereji ya nje. Je. ile mifereji ya ndani fedha zake zitakwenda upande gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kama ilivyosema hizi kamati kutakuwa na tunaita *water kiosk* ambazo zitakuwa zinaendeshwa na wananchi wenyewe na fedha hizi zitakuwa zinaendesha ile jumuia. Hizi fedha za ndani zitaendelea kuja kwenye Mamlaka ya Maji na zitatumika kwa shughuli nyengine za kuendeleza huduma za maji katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.. Kwa kweli maji tunayataka na njia tunazitaka. Tumetengeneza njia kwa awamu ya kwanza kule kinuni kwa kweli hivi sasa hali mbaya mpaka watu hawanielewi, njia hamna kwa kuchimba mabomba.

Sasa tunataka kufanya ukarabati wa awamu ya pili kuziba yale mashimo na kutengeza kurudisha katika hali ya kawaida. Lakini mle mimi sijaona *branch* zilizochimbwa. Kwa hivyo, kwanza tukimaliza wakija kuanza kuchimba ananihakikishia ile njia yangu itakuwaje manusura yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli maji tunayataka na huku ili maji yafike inabidi wakati mwengine, sio wakati mengine, wakati wote tukate barabara ama za lami au hata hizi za kawaida.

Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wa Jimbo la Magogoni maeneo ya Kinuni huko, kwamba maeneo yote ambayo yamechimbwa kwa ajili ya kufukia hii mitaro, basi Mamlaka ya Maji baada ya kukamilisha kazi zake yatawaweka sawa ili gari ziweze kupita na kutoa huduma kwa wananchi kama kawaida, wala wasiwe na wasi wasi. Namthibitishia Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi, kazi hiyo ya kurudisha maeneo hayo kama yalivyokuwa ili njia zipitike itafanywa na Mamlaka ya Maji.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa mifereji iliyo nje itakuwa inalipiwa, na kwa kuwa katika Wizara ya Afya kuna msamaha wa wale waliokuwa hawana uwezo. Je, hii mifereji ya nje itakayolipiwa kwa watu wasio na uwezo kutakuwa na njia gani ya wao kupata maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwanza nataka niseme maji hayalipiwi, tunachangia tu kiasi kidogo cha fedha ambazo zitakuwa zinasaidia kuendesha shughuli zetu za upatikanaji wa maji kwa uhakika.

Nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi na wananchi wote, kwa kweli tunajua uwezo wetu wa kipato unapitana, wako tunaopata shilingi moja kwa siku, wako tunalala kwa chai tu. Kwa hivyo, ukweli kwa wale wananchi ambao hawana uwezo kwa kutumia hii mifereji ya nje wataendelea kuwa na utaratibu mzuri kuhakikisha hawapati bughudha ya kukosa maji. Wasiwe na wasi wasi juu ya jambo hilo.

Nam. 15

Usajili wa Meli Zanzibar

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji - Aliuliza:-

Hivi karibuni tulipata taarifa kwamba MV BARAKAALE I ambayo inamilikiwa na Mdjibout na Mwingereza ilinusurika kutekwa nyara na maharamia wa Kisomali, baada ya kupata usaidizi wa Marekani. Taarifa hiyo ilieleza kwamba meli hiyo ilisajiliwa Zanzibar.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna utaratibu gani wa kuzifanyia usajili meli za aina hiyo hapa Zanzibar na husajiliwa kwa muda gani?

(b) Serikali inafaidika vipi kimapato kwa usajili wa meli za aina hiyo?

(c) Je, upo utaratibu wa kuzilazimisha meli zinazosajiliwa Zanzibar kuajiri mabaharia kutoka Zanzibar?

(d) Je, ni meli ngapi za kigeni zimesajiliwa Zanzibar kufikia sasa?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu majibu ya uhakika Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 15 a, b,c na d kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Meli ya Barakaale I iliwahi kupeperusha bendera ya Tanzania kwa kipindi cha miezi 3 kuanzia tarehe 1 July 2009 hadi tarehe 30/9/2009. Baada ya kusajiliwa katika usajili wa kimataifa wa Zanzibar kwa kupitia Mwakilishi wa Serikali aliyeko nchini Dubai. Mnamo tarehe 21 Februari, 2010 meli hiyo ilipata msukosuko wa kutaka kutekwa nyara na maharamia huko Somali. Meli hiyo ilikuwa haiko kwenye usajili wa Zanzibar kwa wakati huo ilikuwa meli hiyo iko katika usajili wa nchi ya Korea ya Kaskazini.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Meli hizo zinazosajiliwa chini ya utaratibu uliotajwa katika sheria namba 5 ya mwaka 2006 ya "*The Maritime Transport Act 2006*" na kanuni za usajili za mwaka 2007. Utaratibu wa

kuzisajili meli hizo kwa ufupi ni kuwa, lazima muombaji awasilishe ombi la usajili pamoja na hati za umiliki wa chombo hicho, pamoja na vyeti vya meli, cheti cha kufuta usajili uliopita pamoja na malipo yanayostahili;

(b) Serikali inafaidika na mapato yanayotokana na usajili wa meli hizo kwa asilimia 65 ya mapato yanayokusanywa, na asiliamia 35 ya mapato huchukuliwa na wakala anayefanyakazi hiyo kwa niaba ya serikali. Mapato hayo yanaingia katika mapato yanayokusanywa na Mrajis wa Meli na baadae kuwasilishwa Serikali Kuu;

(c) Hakuna utaratibu wa kuzilazimisha meli zinazosajiliwa Zanzibar kuajiri mabaharia kutoka Zanzibar. Kwani asili ya usajili wa meli za kimataifa ni kutafuta uhuru wa kuajiri mabaharia kutoka sehemu yoyote duniani; na

(d) Jumla ya meli 47 zimesajiliwa hadi kufikia mwezi Machi, 2010 na jumla ya shilingi 38,343,298.06 zimekusanywa kwa shughuli hiyo.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu ya waziri ambayo yameniridhi, ila nina swali dogo moja tu. Kwa kuwa tatizo la utekwaji nyara meli na maharamia limekuwa likiongezeka siku hadi siku. Juzi tu hapa katika bahari ya Pemba tatizo kama hili lilikuwepo, lakini kwa msaada wa meli za kigeni tuliweza kui-*save* ile hali.

Je, serikali ina utaratibu gani wa kuona sasa kwamba ulinzi katika bahari zetu unaimarishwa na pengine kikosi chetu cha KMKM kupewa nyezo na elimu ya kuweza sasa kufanya doria katika bahari badala ya kukamata magendo ya karafuu tu, ili kudumisha usalama katika bahari yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba sasa hivi kuna tatizo kubwa la kidunia la uharamia wa meli na hili sio kwa Zanzibar tu, pengine sisi tuko afadhali kidogo kuliko wenzetu. Meli zikipita katika ukanda wa Somali nakupandia juu huko zikipita salama zinakuwa ni afadhali. Mpaka sasa wenye meli nyingi za kimataifa wamebadilisha mkondo wa kupita kujia huku kwetu na imeongeza gharama za usafiri kwa wenye meli.

Lakini kwa upande wa Zanzibar tuliwahi kusajili meli mwaka 2007 ambazo zilikaribia kutekwa nyara inaitwa Mavuno I na Mavuno II, katika ukanda huo huo wa Somali. Na hivi juzi kama alivyosema Mheshimiwa katika ukanda wa

Pemba hapo Mombasa kuna meli moja ya *Cyprus* inaitwa *NORAD Neptune* ilitaka kutekwa nyara lakini bahati nzuri sio meli za Kimataifa zilizosaidia isipokuwa ndege ya Majeshi ya Ulaya ndio ambayo imesaidia kufanya shughuli hiyo.

Sisi tunajiimarisha lakini uwezo wetu sio mkubwa sana. Kwa sababu kwa mujibu wa takwimu nilizozipata ili chombo cha KMKM kifike pale ambapo pana meli yetu, ile meli basi ilikuwa inahitaji mafuta lita 11,000. Sasa ni pesa nyingi mno. Tunashauriana na watu wa Wizara ya Fedha na Tawala za Mikoa, kwa sababu kwa mujibu wa sheria ya *Maritime Act* imempa mamlaka Waziri mhusika wa Mawasiliano na Uchukuzi kuweka gharama za *Star Charge*, tukikubaliana hizo zinaweza zikatusaidia kuweza kupata fedha za kufanya *patrol* katika ukanda wetu huu wa Zanzibar. Lakini ni suala zito la kimataifa ambalo tunalijadili katika mikutano ya kikanda na ya kidunia kulimaliza lakini ni suala kubwa.

Sasa hivi nchi ya Marekani imeshatoa agizo katika kikao kilichopita cha *IMO* kwamba, mali za Wasomali zitapekuliwa zaidi kuangaliwa uhalali wake bila ya kujali zilizo nchi gani. Kwa sababu ya tatizo hili la utekaji nyara.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika maelezo ya Mhe.Waziri ametuambia kwamba usajili wa meli wa aina hii unaipatia mapato Zanzibar. Ni jambo zuri. Pia ametuambia kwamba meli hii ya MV. BARAKAALE I ilisajili kwa muda wa miezi mitatu tu, halafu ikienda kufanya usajili Korea. Maana yake ni kwamba sasa mapato yale tushayakosa.

Je, kuna sababu yoyote ambayo anaijua yeye iliyoifanya meli hiyo kuacha kuendelea na usajili wetu na kwenda kutafuta usajili Korea.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba, hizi meli au wenye meli wana utaratibu wao wenyewe wanaojipangia kwamba anaweza kusajili Zanzibar akakaa miezi mitatu akaondoa akaenda nchi nyengine na ni mzunguko wa kidunia. Sisi sasa hivi tunae wakala wetu ambaye anatufanyia usajili yuko Dubai, lakini pia kuna mwengine ametuomba yuko nchi nyengine na ametuambia ana meli nyingi ambazo anataka kusajili kwetu Zanzibar.

Kwa hivyo, na huyu BARAKAALE I alipokuja Zanzibar haikuwa meli kwamba ndio kwanza mpya imekuja kujisajili Zanzibar. Wametoka walikotoka inawezekana pengine petu sisi ulikuwa usajili wa saba au wa nane na akaelekea Korea. Wale walivyotekwa walisema kwamba ni Tanzania kwa sababu pia waliona wanawaokoa Wamarekani wasingelikuwa tayari kuwaokoa kama wao

wako chini ya Korea. Kwa hivyo, wakatumia jina la Tanzania kwanza ili waokolewe, lakini baadaye hata huyo Mmarekani mwenyewe akathibitisha kwamba ni Mkorea, lakini wakati huo wameshaokolewa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, dunia hivi sasa imo katika vita vikubwa vya uharamia ambavyo tunategemea kwa asilimia kubwa hupunguza uwezo wa nchi kujiendeleza kutokana na umasikini unaosababisha kuongeza bei kutokana na gharama za usafiri wa huduma mbali mbali.

Lakini kwa kuwa Zanzibar tuna bahati ya kuwa na Kikosi chetu cha KMKM, na mara nyingi katika kupitisha bajeti yetu hapa huwa kuna kelele kuwa vikosi hivi vinapewa pesa nyingi, lakini kumbe faida yake hatuifahamu. Mimi Mhe. Spika, swali langu lipo hapa.

Kwa kuwa wenzetu wa KMKM wana uwezo wa kufanya kazi nzuri lakini nyezo ni suala la mwanzo ili wafanye kazi vizuri. Hivyo serikali ina mpango gani wa makusudi kwa kuzingatia hili suala la kimataifa lililotokea kutafuta boti za kisasa zenye mwendo wa kasi kuliko hizo za maharamia.

Pili, kwa kuwa askari wetu ni vyema wakapatiwa mafunzo ya kuendeleza juhudi zao za kumiliki harakati za kiharamia zinazotokea duniani. Wizara au serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapatiwa mafunzo maalum ya kuhakikisha kuwa wanajihami pindi likitokea tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, katika majibu ya nyongeza nilisema kwamba, kutokana na tatizo hili tutaandaa kikao kati ya sisi, Wizara ya Fedha na Tawala za Mikoa kuangalia jinsi ya vikosi vyetu kuwa tutaviimarisha vipi katika suala la ulinzi. Lakini nina hakika kwamba askari wetu uwezo wanao wa kukabiliana na tatizo hili isipokuwa bado ni nyezo na vifaa vyengine.

Lakini pia naomba niliarifu Baraza hili kwamba, hili suala la uharamia wa meli liko katika hali ya juu sana. Kwa sababu hawa wanaoteka nyara meli, wakiiteka nyara meli yako wanaposema uwape dola 20 milioni basi wana masharti yao. Kwanza fedha yenyewe isiwe ya dola mia, iwe 20 au 50, halafu la pili lazima iwe pesa kuukuu sio ukaichukue benki mpya. Kwa hivyo, inawezekana ikawa umechukua gunia zima la dola unawapelekea, wanakwambia nipelekee pahali fulani ukifika niwekee hapo.

Nimekutana na huyo mwenye MV. BARAKAALE I anasikitika fedha anazo anaweza kuchukua benki lakini hizo hawazitaki wanataka zilizotumika tena

zisizidi shilingi 50, yaani 20 au dola 10 ndio wanazozitaka wao hawataki za mia mia kwa sababu zao wenyewe wanazijua. Nafikiri wanaona wasije wakatekwa kwa fedha mpya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuongezea swali la nyongeza au majibu ya nyongeza kama alivyojibu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi. Amejibu vizuri sana.

Mimi nataka kuongezea kidogo tu. Katika suala zima la kukabiliana na maharamia kwa upande wetu Zanzibar, sisi vile vile ni Tanzania. Kwa hivyo, katika masuala haya ya uharamia hatutumii tu vikosi vyetu vya KMKM peke yao katika suala zima la kulinda visiwa vyetu.

Hivi karibuni yalipotokea masuala ya uharamia na wakakimbilia katika visiwa vya Pemba, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambalo kuna Kikosi cha Maji lilishirikiana na vikosi vyetu, lakini vile vile kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha kwamba wanaangalia katika maeneo yote, na katika eneo lote la anga ya Tanzania au bahari ya Tanzania ikiwemo Zanzibar, ilifanywa *patrol* hiyo na hivi sasa suala hilo linashughulikiwa kwa pamoja.

Kwa hivyo, wananchi wasiwe na wasi wasi suala hili la uharamia kwa upande wa Zanzibar tunalishughulikia Tanzania nzima. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 44

Kampuni ya Kuzalisha Maji ya Kunywa Pemba

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Pemba Bottlers Company Limited (PBMCL) ni kampuni ya wajasiriamali wazalendo iliyoanzishwa kisiwani Pemba kwa ajili ya uzalishaji wa maji safi ya kunywa, kupunguza umaskini na kutoa ajira. Mradi huo umesajiliwa na *ZIPA* chini ya kifungu cha Sheria No. 12 (*Zanzibar Investment Promotion Act 2004*) na imesajiliwa kuwa Kampuni, tarehe 06 Septemba, 2007. Kampuni hiyo imechimba kisima kimoja chenye maji yaliyothibitishwa ubora wake na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) na Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Lakini mpaka leo Kampuni hiyo haijapewa Hatimiliki ya eneo la Mradi na hivyo imeshindwa kuanza uzalishaji.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna tatizo gani la kiufundi lililokwamisha kutolewa kwa hati hiyo?

(b) Kwa kuwa kampuni imesajiliwa lakini imeshindwa kuanza kazi, huoni kuwa hali hiyo inavunja moyo wawekezaji wazalendo, inaitia hasara kampuni hiyo, inaikosesha mapato serikali pamoja na kuzuia ajira zilizotarajiwa?

(c) Je, kama hayo yote umeyaona, wizara yako itachukua hatua gani kulikwamua suala hilo?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 44 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba mwekezaji wa Kiwanda cha Maji pale Pemba bado hajapatiwa hati ya kumiliki ardhi. ZIPA wanalijua hilo na inafanya kazi pamoja na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ili kumtafutia hati mwekezaji huyo. Suala la kuvunjika moyo inategemea hati anayoitaka ana makusudi nayo gani;

(b) Kwa upande wake mwekezaji huyu aliwasilisha mradi ambao unasema, mtaji wa mradi wake utatokana na *cash* ambayo anayo mwenyewe, lakini pia na mikopo. Lakini hakuainisha kwamba anatarajia hati hii ndio imsaidie kupata mikopo. Kwa hivyo, kwa kuwa hakuainisha, uchelewaji wa hati hii kweli unamvunja moyo katika utendaji wa biashara yake; na

(c) Hatua inayochukuliwa na wizara yangu kama nilivyosema, *ZIPA* inafanya kazi na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuhakikisha kwamba mwekezaji huyo anapatiwa hati yake. Lakini kubwa zaidi ni kuwaelimisha wawekezaji hasa wenyeji wa hapa ndani, kuwa wawazi wakati wanapowasilisha miradi yao ili tuweze kuwasaidia vizuri. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu a na b. Katika majibu yake alisema kwamba wawekezaji hawakuwa wazi katika kueleza kuwa mikopo hiyo wataipata baada ya kupewa hatimiliki.

Kwanza nataka kumuuliza Mhe. Waziri. Kweli yeye hajui kwamba mabenki hayatoi mikopo bila ya hatimiliki ya ule mradi unaofanya.

Suala la pili namuuliza kwamba. Katika taratibu za *ZIPA* ni muda gani wa chini kabisa ambao mwekezaji akishakumaliza taratibu za *ZIPA* angetarajiwa kupatiwa hatimiliki ya ardhi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, benki wana aina nyingi za mikopo. Wanaweza wakatumia hati ya mradi, wanaweza wakatumia hati ya nyumba na wanaweza wakatumia hati nyengine kama watakavyokubaliana na mkopaji.

Lakini muda unaotakiwa ili mwekezaji apate hati kwa ukweli ni kwamba, mara baada ya mwekezaji kupata hati ya muda ya uwekezaji, basi hautakiwi kuvuka muda mkubwa mwekezaji anatakiwa kupata hati yake. Lakini pia inategemeana na sheria na kanuni, au sheria na miongozi ya wizara nyengine tofauti na yangu, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Siwezi kuingia kwa undani nikasema mambo ya wizara nyengine, lakini sisi ndani ya *ZIPA* haichukui hata miezi miwili mtu anapewa hati yake ya muda ya kufanya mradi wake. Muda wa kupata hati inategemea miongozo ndani ya wizara nyengine.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikemea sana kulingana na wawekezaji wa miradi mbali mbali kuwekewa vikwazo vikubwa vya kuleta miradi au kutekeleza majukumu yao ya uwekezaji ili viondoshwe.

Je, Mhe. Waziri atanambia nini kulingana na hao watendaji wa wizara hii kuwawekea masharti makubwa ya malipo wawekezaji ili wasije kuwekeza. Hatua gani anachukua Mhe. Waziri kwa watendaji wake wanaoshiriki kufanya mambo kama hayo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kama Mhe. Mwakilishi alifuatilia vizuri nilijibu jibu mama kwa maeneo mawili, ndani ya wizara yangu na ndani ya wizara nyengine. Nilijibu kwamba ndani ya wizara yangu si zaidi ya wiki tatu mwekezaji tayari anakuwa amepewa *interim certificate.* Kwa hiyo, ndani ya wizara yangu hakuna watendaji ambao wanaweka vikwazo.

Lakini kama tunavyojua kwamba *ZIPA* kwa jina inaitwa *One Stop Centre* ingawa kuna majina mengi ambayo inapewa. Hii inatokana na kwamba watendaji ambao wanakwenda *ZIPA* katika Kamati ya Utekelezaji *(Technical Committee)* ambao wanatoka na wizara au taasisi nyengine hawapewi mamlaka kamili ya kufanya maamuzi. Wanakaa katika kikao cha kujadili miradi, inajulikana kwamba mradi unataka ardhi, mradi unataka wafanyakazi wapewe vibali vya kuishi nchini, mradi unataka mambo yote. Lakini bado watendaji wanaoletwa hawapewi mamlaka kamili na taasisi zao.

Kwa maana hiyo, baada ya mwekezaji kupewa *interim certificate* bado taasisi nyengine zinafuata mlolongo wa sheria zao ili mwekezaji atimize yale ambayo

anayataka. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kwamba *ZIPA* watendaji wanaokwenda ile kamati inapewa mamlaka kamili ya kufanya maamuzi.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mtoa kibali cha kuanzisha mradi ni taasisi nyengine na mtoa kibali cha kumiliki ardhi ni taasisi nyengine. Je, Mhe. Waziri, huoni hii ndio sababu ya kuzorotesha miradi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika swali la nyongeza la pili, nakubaliana nae kwamba kwa sababu kamati inayopitisha miradi haina mamlaka kamili ndio sababu ya kucheleweshe miradi. Nikasema kwamba nawaomba taasisi nyengine maafisa wanaokwenda kwenye kamati hii wapewe mamlaka kamili, matumizi ya ardhi yajulikane. Kwa hiyo, mradi unapopitishwa ajulikane mtu anakwenda eneo gani na hati yake inapatikana kwa muda gani.

Hoja za Serikali

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2010/2011 – Wizara ya Fedha na Uchumi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tulikubaliana jana kwamba asubuhi ya leo tufanye majumuisho, isipokuwa kuna wachangiaji wangu wawili ambao ndio wamebaki hapa naomba tukubali kwamba hawa wamalize tena tumuombe Waziri ili kufanya majumuisho.

Kwa hali hiyo basi, naomba nimkaribishe Mhe. Omar Ali Shehe na baadae Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Mhe. Spika, nakushukuru na nianze kwa kumshukuru *Allah* ambaye ametuamsha tukiwa wazima wa afya leo hii na kuwepo hapa ili kushughulikia shughuli ambazo zitaleta maendeleo kwa wananchi wetu ambao wametuchagua. Lakini shukrani za pekee zije kwako kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa mwisho katika bajeti hii kwa mwaka huu na ambayo ni bajeti ya mwisho ya kumaliza miaka 10 ya awamu ya 6. Nakushukuru sana.

Mhe. Spika, naomba pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe ambao kwa niaba yao ndio nasimama hapa. Lakini pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi, Dk. Mwinyihaji Makame kwa kuwasilisha hotuba yake.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake ndefu kwangu mimi kwa kuwa ni mwaka wangu wa tano kuwepo hapa, ilikuwa ni kwa mara ya kwanza kuweza kuona hotuba ndefu ya aina hii, lakini kwa kweli ilikuwa na sababu ya aina yake na tumeipokea. Lakini pia shukrani zangu za dhati pia ziende kwa watendaji wote wa wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Kwa kweli wanastahili pongezi.

Mhe. Spika, pia nitoe shukrani za dhati kwa Waziri Kivuli wa kambi ya upinzani kwa hotuba yake ambayo nayo aliiwasilisha baada ya Mhe. Waziri. Kwa kweli mimi naiunga mkono mia juu ya mia.

Mhe. Spika, tukianza na ukweli kwamba bajeti ni nyenzo ambayo inaelekeza njia ya kuweza kupata mapato, yaani namna ya kukusanya na jinsi ya kuzipanga zile rasilimali ambazo unazo kama ni chache au kama ni nyingi ili ziweze kuleta maendeleo katika nchi yako.

Lakini wataalam fulani waliwahi kutupa elimu sisi kama wawakilishi. Walikuwa wanatuambia ukitaka kuiangalia bajeti na kui-*assess* kwamba bajeti hiyo ni nzuri au ni mbaya, basi kuna baadhi ya vigezo inabidi uviangalie.

Lakini kimoja muhimu ambacho ndio hasa kinacho-*determine* sifa ya bajeti ni kwamba je, bajeti hiyo inahamasisha ukuaji na uendelezaji wa uchumi? Hicho ndio alichotuachia mhadhiri wetu Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kutupa mafunzo nyakati tofauti wakati alipokuwa anatufunza jinsi ya kuiangalia bajeti.

Kwa hiyo, mimi kwa kiasi niliitazama hii nikaisoma na vitabu vyote viwili, nikarudia na bajeti za nyuma nikaona jinsi ukuaji wa uchumi unavyokwenda na jinsi bajeti yenyewe inavyokwenda, nikaona kwa kweli sisi kama Zanzibar bado hatujafikia kuwa na bajeti ambayo inahamasisha ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo katika uchumi wetu. Hicho nimekiona bado kabisa hatujakifikia. Sababu labda zipo ni nyingi sana, lakini basi ni jukumu letu kuona kwamba ipo haja siku moja na sisi tuwe na bajeti ambayo itakuwa na sifa ya kuitwa bajeti ya nchi.

Mhe. Spika, nimesoma katika kitabu juhudi mbali mbali zilizoelezwa jinsi ya kuimarisha mapato. Lakini nikirudi mwaka wa nyuma katika bajeti kama hii ambayo mimi kwa uono wangu ilikuwa nzuri zaidi, ilikuwa fupi, lakini ilikuwa imepangika na ilikuwa inaeleza ukweli zaidi.

Mhe. Spika, katika kitabu cha bajeti ya mwaka uliopita Mhe. Waziri alitueleza changamoto zinazotukabili katika uchumi wetu kukua. Hayo yapo katika kitabu cha bajeti cha mwaka uliopita ukurasa wa 19 aya ya 33 naomba ninukuu.

Aya ya 33:

> "Mbali ya mafanikio tuliyoyaonesha mwaka ule kuhusiana na uchumi wetu bado changamoto za ndani na za nje zinaathiri ukuaji endelevu wa uchumi wetu. Miongoni mwa changamoto za ndani ni pamoja na kasi kubwa ya ukuaji wa idadi ya watu, uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula, mifugo na samaki, uchanga wa sekta ya viwanda, uchanga wa sekta ya fedha na kiwango cha chini cha usafirishaji bidhaa nje ya nchi".

Mhe. Spika, kwa kweli hapa mimi nilitaka niipongeze wizara kwamba ilikuwa kweli kabisa ilikiona kile kitu ambacho kama ni changamoto. Sasa kwa uono wangu ni kwamba kama bajeti ile hatukufanya labda vizuri kwa kuweza kurekebisha zile changamoto ili tufike kwenye maendeleo, basi bajeti yetu ya mwaka huu ingekuwa imelenga huko. Lakini kwa kweli bado haijajikita katika kutatua zile changamoto ambazo ndizo zinazoelezwa na serikali kwamba bila ya kuzitatua hizi basi uchumi wetu hautaleta maendeleo.

Mhe. Spika, ni jukumu la serikali kuona kwamba zile changamoto bado zipo ingawa kwenye bajeti hii hatujaelezewa, lakini mimi naamini kwamba bado zipo na ndio maana uchumi wetu haujakua. Ni jukumu letu basi kuona kwamba tunazitafutia ufumbuzi hizi changamoto ili uchumi nao uweze kukua.

Kwa sababu Mhe. Spika, bajeti zetu ya mwaka jana na ya mwaka huu zote zina nakisi kwa maana ya kwamba kile tunachokusanya ndani basi hakimudu hata kufidia yale matumizi ya ndani ya nchi yetu.

Kwa mfano, mwaka 2009/2010 bajeti yetu ilikuwa milioni 412,605,000/= lakini makusanyo yetu yalikuwa ni milioni 409,099,000/=. Kwa hiyo, pale kulikuwa na nakisi na tuliambiwa ni ya milioni 3,506,000/=. Mwaka huu nakisi imekuwa kubwa zaidi, mapato yamepungua nakisi iliyopo sasa ni ya milioni 6,000,000/=.

Sasa hivi tunajiongezea deni letu la ndani. Kuna kifungu kimeeleza kwamba deni limekua kwa sababu ya nakisi iliyokuwepo katika bajeti na safari hii ni zaidi. Kwa hiyo, tunaendelea kujiongezea deni. Ili tuone kwamba uchumi unakua kweli kama data zinavyoeleza, mimi kwa muono wangu nataka tufike pahala tuseme basi sasa angalau haya matumizi ya ndani hatutegemei tena fedha ya mfadhili, tunaweza wenyewe kujikimu. Hapo kidogo tutakuwa tumesema tumepiga hatua. Lakini bado hali ya mwaka jana na ya mwaka huu si ya kuridhisha.

Si hivyo tu, mwaka jana tuliambiwa serikali inafanya juhudi kubwa za kuimarisha mapato yasiyo ya kodi. Kimeundwa kitengo katika mawizara na

mambo kama hayo. Lakini ukija ukitazama bajeti kwa mwaka huu kuna *minus* ya mapato ambayo yatapatikana kutokana na vianzio hivyo sijui ni kwa sababu gani. Ikiwa tumeimarisha namna ya kukusanya lakini tutakuwa tumepunguza mapato katika eneo hilo. Nilikuwa naomba hapa Mhe. Waziri aje atueleze labda kuna sababu maalum ambayo imesababisha hilo.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa nipewe maelezo na Mhe. Waziri ni kuhusiana na fedha ambazo tunazipata kama mchango wetu wa asilimia 4.5 kutoka kwa wenzetu wa Tanzania Bara, fedha zinazoitwa *GBS money (General Budget Support).* Niko na gazeti Mhe. Spika, lakini madhumuni yangu ni kunukuu kifungu ambacho kinaelezea shughuli nzima hiyo inayohusiana na fedha hizo zilivyopatikana mwaka jana na zitakavyopatikana mwaka huu.

Mwaka 2010/2011 serikali inategemea kupokea shilingi bilioni 821.6 kama ni misaada ya mikopo ya kibajeti, ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.3 ambazo zinazotarajiwa kwa mwaka huu wa fedha ambao tuko nao. Sababu iliyotolewa kwa nini fedha za mwaka huu zimepungua ni kwamba ipo kwenye gazeti hapo la Mwananchi nafikiri ukurasa wa 6 kama mtapenda kuiangalia zaidi labda mimi nitakuwa sikufahamu mtakaponipa maelezo. Wanasema kwamba naomba kunukuu:

> "Fedha ambazo zilitarajiwa zitiwe katika kifungu cha *GBS money* kipindi hiki hazikutiwa kwa sababu zilitolewa fedha zile zikatiwa katika fedha za mwaka jana kwa ajili ya kushtua uchumi".

Mhe. Spika, Mhe. Waziri mwaka jana alituambia kwamba kwa sababu ya msukosuko wa uchumi, kamati zimeundwa na mambo tele yatafanyika lakini wenzetu **wakapata pesa kushtua uchumi wao nyingi sana.** Sisi kama serikali Mhe. Waziri naomba atueleze, sisi tulipata ngapi. Sasa hivi *GBS money* imepungua kwa sababu ilipelekwa mwaka jana kwa ajili ya kushtua uchumi. Hili tatizo la uchumi wa dunia lilitukumba sote kama Tanzania. Je, sisi katika bajeti yetu hiyo tuliongezewa nasi chochote. Hilo ni moja.

Lakini jengine pale inapokuja tukazungumziwa kwamba sasa serikali yetu nayo itakuwa na uwezo wa kukopa ambalo bado linaonekana na kambi yangu kwamba hilo ni gumu kwa masharti ambayo yamewekwa. Lakini mwaka huu wa fedha katika bajeti ya Tanzania Bara mbali ya zile bilioni nyingi tu ambazo watapata kwa *GBS money* ambao sisi kule ndio tutapata asilimia 4.5, kuna trilioni 2.4 nyengine mpya hizo zinazotokana na misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo ambazo na sisi tunazo *Alhamdulillahi* kidogo zipo hapa Mhe. Waziri ametueleza.

Mhe. Spika, mimi napata mashaka sisi kama Tanzania tunapewa misaada hii kwa jina moja na huku hatuna asilimia 4.5, sisi sijui zile zetu huwa zinatolewa vipi, lakini wenzetu wanapata hela nyingi.

Mhe. Spika, katika mapitio ya utekelezaji wa MKUZA unaonekana kukwama na kutokufanikiwa katika maeneo yake kwa sababu ya ukosefu wa fedha wa kutekeleza mpango ule wa maendeleo. Lakini wenzetu wanapata hela nyingi sana kwa ajili ya kutekeleza MKUKUTA na pengine wao wamepiga hatua zaidi. Labda Mhe. Waziri pia anaweza akaja akatupa sisi MKUZA hali halisi ikoje kwa kuangalia lile la mwanzo kabisa la kuondosha umaskini uliokithiri kwa mwananchi wetu. Maana yake kwa kadri tunavyoona tunakuta bado wananchi wetu ni maskini. Hatuna data za karibu lakini tukitegemea zile zilizopita za *House Budget* Survey bado Wazanzibari walio wengi ni maskini waliokithiri.

Kwa hiyo, labda atakapokuja Mhe. Waziri atatuambia. Sitaki nipelekwe kwenye huduma za jamii, skuli, huku nakubali kabisa moja kwa moja. Lakini hili la mlo ambalo ndio *base* niambiwe vipi wananchi wetu wa Zanzibar kwa kutekeleza MKUZA wa miaka mitatu wamefaidika.

Sasa niko karibu sana kukubaliana na rai ya Mhe. Waziri Kivuli wangu kwamba tuwe na kofia zetu za kuomba tofauti. Au kutokana na udogo wa nchi yetu na rasilimali tulizonazo ndio tunapewa na sisi mikopo na misaada kidogo basi tuelezwe. Lakini *wallahi* inatia huzuni, wenzetu sasa hivi wanakwenda kwenye trilioni 3.4 wakikusanya pesa zote za wahisani. Sisi bado tuko nyuma sana na hizi pesa hata kama mikopo tunakuja kulipa.

Maana yake wenzangu kila siku wanasema fedha huchuma fedha, lakini nguvu zinachuma kijio. Kwa hiyo, hata kama tutakopa lakini tutafanya mambo ya maana tutaweza kuzilipa. Lakini labda uwezo wetu wa kukopa unakuwa hauridhishi nikilinganisha na hawa wenzetu. Mhe. Spika, hapo ningependa nipatiwe maelezo vile vile.

Mhe. Spika, jengine ambalo linatukwaza sana ni suala la mambo yetu yanayohusiana na matatizo ya Muungano. Katika hili Mhe. Spika, mimi naomba nianze kwa kunukuu maneno ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Mhe. Spika, nakushukuru kwanza kwamba ulinipa mwaliko wa kwenda kuhudhuria sherehe za Mapinduzi Pemba na nilikwenda na nilifaidika kwa kiasi fulani. Kitu ambacho nilikipenda ni jinsi ambavyo Mhe. Rais aliutaja Muungano huu. Naomba ninukuu ni katika kitabu kile ambacho tulipewa cha hotuba yake ukurasa wa 33.

> "Ndugu wananchi, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni ubia wa nchi mbili huru zilizoamua kuungana zikitegemea ushirikiano utakaoleta maendeleo zaidi kwa wananchi wa pande zote mbili".

Haya ni maneno mazito, Mhe. Rais kamaliza kila kitu. Kwa mnasaba huo Muungano huu una dhima kubwa ya kuhakikisha kuwa kila upande unawezeshwa kutekeleza dhamira hiyo kwa wananchi wake. Mhe. Spika, hali ilivyo sasa mimi nina wasi wasi kwamba haya tuliyoelezwa na Mhe. Rais, hayapo, upande mmoja unaonekana kutubinya ili uchumi wetu usiendelee na kwa maana hiyo kuwaweka wananchi wetu wa nchi hii ya Zanzibar katika hali ngumu.

Mhe. Spika, matatizo ya Muungano ni mengi sana na karibuni tu Mhe. Waziri mkubwa wa Serikali yetu ya Zanzibar tulikuwa naye katika shughuli zetu za kazi mimi nilimnukuu akisema kwamba "Jamani huo msukosuko wa uchumi huko uliko na mambo mengine, sisi humu ndani ya nchi Zanzibar msukosuko wetu ni Katiba na mambo ya Muungano. Haya ndio yanayotuathiri na ikiwa tutakuwa wajasiri wa kuweza kuyaweka sawa haya matatizo yetu mengi yataondoka". Huyo alikuwa Mhe. Hamza Hassan Juma akiwa Hoteli ya Bwawani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi siku nyingi kila nikisimama hapa Mhe. Spika, huwa nazungumzia suala la *Joint Finance Commission*. Kwa kuwa sasa tunafikia tamati ya miaka mitano basi sitafanya haki kama sitalihitimishia hapa. Lakini tunapoelezea masuala haya wakati mwengine Mawaziri wanaripuka "Oh! Mkoo nyinyi wabunge".

Mhe. Spika, mimi nashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu walinichagua nikenda Bungeni, kama mtakwenda kutazama *hansard* za Bunge mnaweza kuangalia mara ngapi Fatma Fereji kaulizia kuhusu suala la *JFC*. Lakini Mhe. Spika, wabunge wote tuliokuwemo nguvu zetu si sawa sawa na serikali, serikali ndio *mas'ul* wa wote haya.

Hata ile tume iliyoundwa ya kurekebisha matatizo ya Muungano huku hawakupelekwa wabunge wala mwakilishi kwa kuwa serikali yenyewe ndio yenye dhamana na ndio *mas'ul* wa haya. Kwa hiyo, msitupeleke huko kwamba wabunge mko, ndio tuko lakini nguvu zetu ni ndogo kuliko serikali na nyinyi mnajua kabisa. Kweli utamfananisha mbunge na serikali haiwezekani, hata wabunge mia huwezi kuwafananisha na serikali, serikali ni dola.

Mhe. Spika, suala hili waziri ametujibu kwa kirahisi tu. Kwanza nikushukuru kwa hatua ambayo imefikiwa na waziri kuona yale ambayo tunayazungumza humu ndani ya Baraza yana umuhimu kutafutiwa ufumbuzi. Mimi nashukuru

sana, mengi ambayo tunayagusa hata kama bado hayajaturidhisha katika utekelezaji wake lakini angalau hatua zimeanza kuchukuliwa. Hilo nashukuru.

Lakini hili la *JFC* Mhe. Spika, maelezo yaliyomo ndani ya kitabu mimi binafsi hayaniridhishi na inanifanya kuiona kama serikali haiko *serious* na hapa ndio kwenye roho yote ya serikali, ndio kwenye mapato.

Mhe. Spika, ripoti hizi nitasema tena na tena toka Agosti, 2006 zimewasilishwa kwa serikali zote mbili. Huku kwetu kwanza tulikuwa tunaambiwa jamani mambo haya si ya kuvamia, sisi tumekubali. Wametafuta washauri elekezi wakashauri serikali yetu nafikiri kwetu kumekaa sawa na wenzetu labda na wao vile vile.

Lakini sasa tukiambiwa wenzetu hawajawa tayari na sisi tumekaa tu tuwasubiri wawe tayari na kwa sababu tunaoumia ni sisi Mhe. Spika, waziri hatutendei haki. Sisi tunachotaka kuona ni mkakati wa makusudi wa kuwaweka wenzetu tunaokutana nao ni binadamu kama sisi. Hivi tukiwaambia jamani suala hili tulizungumzeni sasa, hebu Tuwaambieni tulizungumzeni kwamba sisi huko wenye nchi yao wanapiga kelele. Tuwasikilize wanasema nini halafu maamuzi sisi tutakuwa nayo. Lakini kwa kuambiwa tu kwamba wenzetu hawajawa tayari ndio ripoti tunayoletewa hapa kwa kweli inakatisha tamaa.

Mhe. Spika, mimi naomba kwa heshima kubwa niliyonayo kwa waziri na watendaji wake na serikali nzima, basi suala hili kwa kweli walipe uzito wa aina yake. Kwa sababu hizo kelele zote za asilimia 4.5 sijui kwenye *GBS*, asilimia 4.5 kwenye mapato ya *BOT* zote zitaondoka. Ninaamini kama maelekezo yaliyotolewa mle yatafuatwa basi tutaweza kukwamuka kiuchumi. Hiyo ni imani yangu na ndio maana ninakuwa naumia sana nikiwa sipati majibu *JFC* inafanya nini.

Walikuja hapa makamishna wa *JFC* na wakatupa semina katika ukumbi huu. Wanasema sisi kazi yetu kutoa ushauri kwa serikali, ni juu ya serikali sasa ku-*act* kwa yale tuliyoyasema, waseme aaa haya hatuyataki au haya hayatufai. Sasa wamekaa hawajarejeshewa majibu na wao wametwambia na serikali zote mbili hakuna hata moja iliyokwenda ikawaambia hata tumepokea lakini labda hivi na vile. Kwa hivyo, hiyo hali kwa kweli inaturudisha nyuma.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuipongeza serikali ni juu ya udhibiti wa matumizi ya fedha, rasilimali ndogo tuliyonayo. Mhe. Spika, katika hili usiwe na wasi wasi mimi ni Mwenyekiti wa Kamati yako ya *PAC* ambao ndio tunapita humo katika mawizara kukagua. Katika suala la matumizi ya fedha hali imeboreka, kuanzishwa kwa mtandao wa *IFMS*, kueleweka kwa sheria za

manunuzi na sheria ya fedha kwa kiasi fulani kumesaidia kuimarisha ubadhirifu wa fedha kwa maana ya fedha *(cash money)* ndani ya serikali yetu.

Hata kama unataka uthibitisho unaweza kuangalia kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utaona katika eneo hilo hali sio mbaya, fedha ndogo iliyopo inatunzwa. Isipokuwa kuna wakorofi wawili watatu kama ilivyo kawaida ya mwanadamu hatuwezi kuwa na mia juu ya mia, lakini mambo sio mbaya.

Mhe. Spika, kuna mambo mawili ambayo sasa nataka serikali ijikite nayo ili tujisifu basi rasilimali zote tulizonazo kama Zanzibar zinatunzwa vyema. Moja linahusiana na *asset register*. Yaani Mhe. Spika, hapa tunazungumzia fedha lakini tayari serikali ina mali ambazo zipo, majengo, magari, mifugo, mashamba na mambo kama hayo. Huku kwenye eneo hili bado hakujakaa sawa.

Tumeshuhudia kama Kamati ya *PAC* watu wakikatiana maeneo ya mashamba ya serikali wakijenga nyumba, tumeshuhudia pia watu wakigeuza mali za serikali kuwa zao zikibabaishwa na mambo kama hayo. Tumelizungumza sana na wenzetu serikali wamelisikia na wamelichukulia hatua. Niwapongeze kwamba wameshakuja na mfumo wa kuweza ku-*register* zile mali na kuziorodhesha, lakini bado hatua iko ya awali ya mwanzo kabisa. Sasa ni muhimu tukahifadhi mali zetu, mtu ambaye hazijui mali zake basi unaweza hata kuibiwa mwenyewe huna habari. Kwa hiyo, ni muhimu kuzifanyia registration na kuzihifadhi.

Lakini la pili ni kwamba sasa serikali imuwezeshe Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa samani *(value for money audit).* Kwa sababu fedha nyingi Mhe. Spika, hizi ambazo tumekusanya ndani na tulichoomba omba na tulichosaidiwa inakwenda kwenye manunuzi au *transaction* maeneo ya kujenga na mambo kama hayo.

Mhe. Spika, haipendezi, jana nilishtuka mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* lakini nikasema doh!, tumefikia mwisho, lakini ingekuwa ndio ya mwanzo kwenda kuifanyia kazi kuitafutia ni jinsi gani jengo lililojengwa Pemba limeanguka. Inakuwaje nguvu na fedha za walipa jasho wa nchi hii zinajengewa jengo linaanguka. Hapa Mhe. Spika, mkaguzi wetu nafikiri amelisikia ni pahala pakwenda kufanya kazi.

Ni wajibu wa serikali kujikita kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuweza kufanya ukaguzi wa samani. Hatuwezi kukaa tukasema kwamba barabara hii imejengwa kwa bilioni moja lakini ikienda ikikaguliwa baada ya siku mbili mashimo tunaambiwa kwamba fedha

iliyotumika sivyo ilivyojengwa. Kwa kweli ili tuwe na udhibiti kabisa wa *resources* zetu basi ningeomba pia serikali ilitizame.

Mhe. Spika, jengine ambalo katika mapato yetu napenda litizamwe ni suala la misamaha ya kodi. Suala hili bado ni tatizo fedha nyingi ambayo inakusanywa nyengine inakwenda kwenye kusamehewa. Mimi nakubali kabisa kwamba tuna wafadhili wetu ambao watakuja kufanya miradi. Vitu ambavyo wanaingiza hatuwezi tukawatoza kodi. Nakubaliana na shughuli za kimaendeleo ambazo zinafanyika inabidi tusamehe kodi.

Mhe. Spika, kuna eneo ambalo linanipa mashaka, ni kuhusu hawa wawekezaji tumetoa muda mrefu sana kwa wawekezaji wetu na tumekuwa tunasamehe kiwango kikubwa cha fedha. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi ushauri wangu ni kwamba serikali ipitie sera hizi za uwekezaji na sheria zake, ili iweze kuona kwamba kama taunaweza kukamua chochote kutoka eneo lile ni muda mrefu tumeuachia. Kwa hivyo, tupunguze na tuboreshe eneo moja lile la *one stop center*, lakini tupunguze misamaha ya kodi. Hilo halito tu-*affect* chochote katika uwekezaji wetu kama kweli mwekezaji ana moyo wa kuja kuekeza katika nchi hii. Tukimuekea mambo yake sawa hapa kwamba hakuna urasimu, lakini basi tunampunguzia kidogo misamaha ya kodi ili tuongeze mapato yetu nafikiri sio baya.

Hivi karibuni Mhe. Spika, nimesikia taarifa, lakini labda Mhe Waziri atakuja kutupa *details* hapa. Katika Wilaya ya Kati masaruji yamesamehewa kodi, zaidi kwa shughuli za maendeleo ya Wilaya ya Kati. Mimi nikawa najiuliza na ninawauliza watu wa kule kidogo kuna shughuli gani? Lakini jibu sijapata. Sasa mimi bado nina mashaka Mhe. Spika, kwamba kuna wajanja wanapita kwenye mgongo huu wa kusamehewa kodi wakitupunguzia mapato yetu. Kwa hivyo, ningeomba sana serikali ijikite katika kuangalia shughuli nzima ya kusamehe kodi kwamba inakwenda kama inavyotakiwa, ili iwe hakuna uvujaji wa mapato wetu.

Jengine Mhe. Spika, ambalo Waziri Kivuli alilielezea na mimi likanishtua ikabidi nitafute kitabu nianze kuingia ndani kufanya kazi. Ni suala lile linalohusiana na *allocation* ya fedha katika vitengo vyetu mbali mbali. Mhe. Waziri Kivuli yeye aligusia juu ya afisi ya vitambulisho. Mimi nikenda kwenye kitabu sikutaka kujiridhisha tu moja kwa moja na hotuba yake na nikajipa kufanya *home work* kidogo kuangalia mbili au tatu kama kweli yale aliyosema yana *logic*. Nikakuta ni kweli, kwa sababu katika afisi hii ya Idara ya Vitambulisho fungu la takrima kwa Unguja na Pemba limepewa milioni 243. nikasema hebu niangalie taasisi nyengine zikoje. Nikenda katika Afisi ya Waziri Kiongozi, katika *section* ya mipango wao wamepangiwa milioni 51. Nikasema hebu niende kwa wakubwa wengine Afisi ya Rais Ikulu mipango

nikakuta milioni 160 na hawa kwangu mimi kama serikali ndio wenye watu wengi wa kuwakarimu, maana yake wana wageni na mambo yote.

Mhe. Spika, vile vile nikasema hebu nitofautishe na vitu vyengine vya huduma kama Idara ya Kinga nzima kwa shughuli zake za Unguja na Pemba basi ina milioni 135. elimu abayo ni kipaumbele chetu hiki, Idara ya Sekondari nzima kwa Unguja na Pemba ambayo imepangiwa milioni 150. Lakini yote hapa asubuhi tulikuwa tunaongelea habari ya maafa na ni mengi katika nchi na kadri hali ya hewa inavyobadilika basi maafa pia yanakuwa mengi. Idara ya Maafa kwa shughuli zake zote imepangiwa milioni 168 loo! Nikasema hili kwa kweli Mhe. Waziri ni lazima atupe maelezo, tuyakubali au hii hatuipitishi. Milioni 243 kwa takrima na kuvinyima vifungu vingine muhimu huku kwa kweli kwenye akili haliingii. Sasa labda kama hiyo takrima ni maalum atakuja kutuelezea tuje tufahamu baadae, mimi naweza kuwa sio mgumu lakini kidogo niliposikia hotuba nilishtuka. Nikenda kwenye kitabu chenyewe nikafanya *home work* ya kuangalia mambo mawili au matatu na nikakuta suala hilo lina mashakili kidogo katika mgawanyo wake.

Mhe. Spika, siwachi kuisifia bajeti ya mwaka jana kila aliyechangia bajeti Mhe. Spika, alikuwa anagusia suala la uvuvi wa bahari kuu. Mwaka jana katika kitabu cha bajeti kwenye matumizi ya fedha za misaada ya kibajeti na huo ni ukurasa wa 53 wa kitabu cha bajeti cha mwaka jana. Kwa kweli naomba Mhe. Spika, ninukuu.

Ukurasa wa 53

> “lengo kuu la misaada ya kibajeti ni kutekeleza mikakati ya kupunguza umaskini”.

Kwa hivyo, mgawanyo wa fedha hizo katika bajeti ya mwaka 2009/2010 umezingatia kipaumbele kwa maeneo yafuatayo:

1. Kuimarisha sekta ya utalii kupitia maendeleo ya miundombinu, mkazo zaidi ukiwa kuimarisha viwanja vya ndege, barabara, chuo cha utalii, nishati na maji safi na salama.
2. Kuimarisha uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji kwa ajili ya masoko ya ndani na nje na kuwa na uhakika wa chakula na kuongeza thamani kwa bidhaa zinazozalishwa kwa kushirikisha sekta binafsi na wajasiriamali wa kati na wadogo.
3. Utekelezaji wa mpango mkuu wa umwagiliaji maji na uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, hivyo ndio vilikuwa vipaumbele na ndio *allocation* ya matumizi ya misaada ya kibajeti ilivyokwenda. Sasa inashangaza kuwa Mhe. Waziri safari hii, kwa kweli alikuwa na mengi maana yake kuweza kufanya *evaluation* ya miaka 10 basi unaweza kuwa umesahau mengine. Lakini basi atakapokuja atuambie, kama kulikuwa na *allocation* ile ya kuweza kushughulikia eneo la uvuvi wa bahari kuu, fedha zile tulizozitenga kule angalau zimefanya kitu gani, au tumebadilisha mawazo hatukuzipeleka tena. Kwa sababu kitabu kinatuambia kwamba mlitenga hela na ilikuwa safari hii tuone tena kwamba eneo lile linatengewa. Lakini kama walivyosema wenzangu hapa pamesahauliwa.

Siku moja Mhe. Waziri Kivuli ali-*comment* hapa kwamba waziri aliyepita nadhani wa mwaka 2004 wa Wizara ya Fedha na Uchumi, alisema kwamba uvuvi unaweza kuipatia nchi yetu nusu ya mapato ambayo inahitajia ikiwa tutaifanyia kazi. Lakini inasikitisha Mhe. Spika, kwamba waziri hilo hatukuliona katika mipango yake likipewa kipaumbele.

Mhe. Spika, naona waziri anatizama saa, sijui nimetumia muda gani? Lakini naomba niende mbio mbio. Mhe. Spika, naomba niisifu pia bajeti hii kwa mambo mawili mapya ambayo yamekuja. Bajeti hii haikutoa ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi, lakini kumeanzishwa mfuko wa majimbo *CDF*, au unategemewa kuanzishwa maana kuanzishwa kwake lazima ipatikane sheria, hilo ni jambo la kupongezwa. Kwa hivyo, ningeiomba serikali ikae kitako vizuri ilitafakari na kuliangalia ni jinsi gani bora ya kuweza kulileta kwenye majimbo, kwa sababu lile lalamiko walilosema wenzangu kwamba wengine walipata na wengine hawakupata. Ni kweli, mimi ni mmoja ambaye sikufaidika kabisa na mfuko huo wala ulikuwa hautajwi na Mhe. Subeit anasema na yeye, lakini tutawamaliza wote. Kwa hivyo, tuwache.

Mhe. Spika, kubwa ambalo naomba niliseme kabla sijamaliza muda wako ni suala la kuanzishwa kwa *Parliamentary Fund.* Mhe. Spika, inatia huruma sana unapomsikia Mhe. Spika, au Katibu wa Baraza ambaye ndiye mtendaji mkuu wa chombo hiki, ambao ni mhimili mmoja wapo katika mihimili mitatu mkuu, anasikitika anasema sasa fedha sina nitafanya nini. Chombo hiki ndicho kinachopaswa kusimamia mafedha yote haya ambayo yanapelekwa serikali kuyaona kwamba yanakwenda sawa. Sio hiyo tu mipango na mambo mengine yote, shughuli zake ni nyingi. Sasa ikiwa bado tutaendelea kugawa hizi pesa kwa chenga chenga, kwa kweli hatukipi hadhi chombo hiki.

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba serikali sasa wakati umefika ikae kitako ianzishe mfuko huu wa Baraza la Wawakilishi, ambao utatoa nafuu katika utekelezaji wa shughuli za kiutendaji wa chombo hiki, lakini pia shughuli za utendaji wa wawakilishi wa wananchi wote wa nchi hii ambao wamo ndani ya chombo hiki.

Mhe. Spika, kwa masikitiko wakati mwengine wajumbe wako au wewe mwenyewe unahitajika kwenda pahala kwa manufaa ya kuja kufaidisha Baraza lako hili, lakini unashindwa. Sipendi niwe mkosefu wa shukrani, nashukuru kwa pale tunapopapata. Wakati mwengine wanafanya haraka sana katika kutuwezesha ili tuweze kufanikiwa. Lakini kwa nini tuwape tabu hiyo, tuanze kumtafuta *accouter general*, tuanze kuzungumza na waziri ili mambo yetu yawe. Mhe. Spika, ni busara sasa kukaanzishwa mfuko mzima huu ambao utahusika na masuala ya Baraza la Wawakilishi, ili kukiwezesha chombo hiki kiweze kufanya shughuli zake vizuri.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitowe shukurani tu lakini pia niombe maelezo ni jinsi ambavyo serikali imeona umuhimu wa wanawake ndani ya chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. Juzi katibu wetu mmoja alitupa *data* inayoonesha idadi ya wawakilishi waliomo na jinsi gani wamegawika na vyombo vyengine. Kwa miaka hii mitano tunayokwenda nayo, asilimia ya wawakilishi wanawake ndani ya chombo chako ilikuwa ni asilimia 23.5 tu, licha ya kwamba kulikuwa na asilimia 30 ambayo ingetakiwa ifikie, hiyo tulikuwa hatukuifikia. Lakini niliposoma maelezo ya kitabu waziri ameeleza asilimia 40 kwa nafasi za kuchaguliwa.

Mhe. Spika, tumezowea humu kutumia lugha nafasi za kuchaguliwa ni za majimboni, halafu kuna *special sit*, kuna nafasi ya kuteuliwa na Rais na mambo kama hayo. Mimi ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja aje kuniwekea wazi ikoje. Kwa sababu unaposema tu nafasi ya kuchaguliwa, kidogo utahisi kuwa ni katika hiyo ya majimbo ndio tukajitahidi huko tufike hapa tuwe asilimia 40. Kwa njia hii naona tutakuwa hatujatendewa haki, maana yake huko kugumu kwenye majimbo. Maana yake basi tuelezwe vizuri, lakini Waheshimiwa Wanawake wenzangu msiogope, tuwe wajasiri na twendeni majimboni, hali tutapambana nayo hivyo hivyo hiyo tutakayoikuta huko majimboni, tuoneshe ujasiri wetu twendeni majimboni.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa mchango wako huo. Wito kwa wanawake wengine kwenda katika majimbo tunakushukuru sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi.

Ningewaomba basi Waheshimiwa Wajumbe wawemo ndani humu ili wasikilize ufafanuzi unaotolewa ili mara baada ya hapo tuweze kupitisha bajeti tukiwa tuko wengi wa kutosha ndani ya ukumbi huu. Naomba sana na watendaji wetu tujaribu kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe warudi ukumbini.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukushukuru sana kunipatia nafasi hii kuweza kusimama hapa nikiwa na uzima wa afya, kuweza kufanya majumuisho ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, katika kujadili hotuba ya mapendekezo ya mpango wa maendeleo na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/11.

Mhe. Spika, pia sina budi na hilo ningelisema mwanzo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa wazima na afya kuja kuchangia hapa. Pia kumaliza mwaka wetu wa fedha kwa shughuli zetu hizi muhimu sana za hapa Barazani.

Mhe. Spika, Waheshimiwa waliotangulia ambao hawakuwahi kulimaliza Baraza hili tunamuomba Mwenyezi Mungu basi awape salama huko waliko na awasamehe madhambi yao yote. Kwa nia njema kabisa wametangulia mbele ya haki na sisi tuko njiani.

Mhe. Spika, kwa kweli michango ya mwaka huu kwa kweli ni ya aina yake. Nikisema ni ya aina yake kwa sababu hotuba imechambuliwa kweli kweli. Ningeanza kumjibu mmoja mmoja na kila hoja Mhe. Spika, ningeomba masaa manne. Maana yake hoja ni nyingi na takriban waheshimiwa wote ni 34 waliochangia. Waheshimiwa Wajumbe 32 wamechangia hapa ukumbini na 2 wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, kwa kweli nawashukuru sana na michango yao wazungu wanasema ilikuwa *very constructive*, lakini zaidi ni kwamba ilikuwa ni michango ya kutaka kujenga, kutuelekeza, kutushauri na hapa na pale kutukosoa kwenye mwenendo wetu. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi nawashukuru sana tena sana. Sisi Wizara ya Fedha na Uchumi ambao ndio wasimamizi wakuu wa bajeti hii ya serikali, kwa niaba ya wizara nyengine tunasema tunawashukuru sana na michango ambayo mmeitoa na ambayo mlikuwa mkiitoa tokea kwenye kamati imetusaidia sana na itaendelea kutusaidia nafikiri kuimarisha shughuli zetu za utendaji pamoja na uandaaji wa bajeti mpya hapo mwakani.

Mhe. Spika, mwaka huu nikisema ni wa aina yake, ni kwamba sikusikia rafiki yangu Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa na lalamiko lake la kila mwaka, ambalo nilikuwa nalisubiri ataniambiaje kuhusu uingizaji fedha Pemba. Nashukuru sikulisikia, kwa hivyo najua mambo yamekwenda vizuri sana. Lazima nipongeze kwa ushauri wake na ufuatiliaji wake.

Vile vile Mhe. Rashid Seif Suleiman yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini huwa kuna mambo ambayo tunayazungumza kule hatukubaliani bado anayaleta hapa, sijui tena kwenye bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi, lakini namshukuru mwaka huu na yeye pia kwa kweli amekuwa *very constructive*. Hii yote Mhe. Spika, inaonesha kama nilivyosema kuwa yale mawazo mnayotuambia sisi tunayasikia, tunayafanyia kazi, tunashirikiana na hasa huu mwelekeo wetu sasa tunaouelekea.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na yeye kwa kweli alikuwa *very exceptional* kwa kuisifu bajeti yetu, kutukosoa na kutuelekeza. Lakini naomba nimshukuru sana Mwenyekiti wa Wenyeviti pia Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alikuwa wa mwanzo katika kuchangia, alitoa niseme joto lake hasa kwenye mambo ambayo angeona yaende vipi?

Mhe. Spika, kwa ujumla kama nilivyosema michango mingi ilikuwa ni ya kutuelekeza, kutukosoa hapa na pale Vipi makosa yetu au twende vipi na yote hayo tunayachukua?

Mhe. Spika, kwa ujumla mimi nimepata mambo makubwa kama 12 hivi, haya ndio mambo makubwa na ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe takriban wengi sana. Kwanza ni suala la mafuta ambalo wemesema tumeliacha kabisa hatukuligusia kwenye bajeti. Mhe. Spika, labda niseme kwa namna moja au nyengine hatukulizungumza nikiri hivyo. Lakini hasa nitagusia baadae, hasa tumeliwachia kwenye sekta yenyewe wakija hapa wakati wa bajeti yao.

Mhe. Spika, pili ni kilimo. Kilimo Mhe. Spika, ilivyokuwa bado ni muhimili wetu mmoja mkubwa sana katika uchangiaji wa pato baada ya huduma. Kwa kweli kilimo kimezungumzwa na waheshimiwa wengi sana na wameshauri kwamba bado wanahisi nguvu zaidi zielekezwe kwenye kilimo. Wanahisi serikali kwa tunavyoichangia sasa kwa asilimia 7.8 bado ni ndogo wanahisi tuongeze zaidi.

Vile vile nataka nilioanishe na suala la karafuu. Pia wametuambia kwamba karafuu tumeitupa. Nitaelezea baadae kwa urefu kabisa, nasema hatukuitupa lakini ni tofauati tu ya ule mwelekeo tu kwamba nguvu zinaelekezwa vipi na nini *role* ya wakulima wenyewe na wananchi wengine kwa ujumla.

Halafu Mhe. Spika, ni suala la uvuvi nalo limezungumzwa kwa upana wake. Bado tumeambiwa kuwa hii ni rasilimali ambayo hatujaigusa, bado samaki kule wanaota ndevu kwa hivyo tushirikiane ili tule samaki kwa wali, tusile wali kwa samaki. Hii ni nyanja ambayo inabidi tui-*address* kwa mapana yake.

Suala la mfumko wa bei Mhe. Spika, ni suala ambalo lilijitokeza na wajumbe wengi sana waliomba kwamba huu mfumko wa bei udhibitiwe kwa namna moja au nyengine. Vile vile suala la *CDF*, nalo wajumbe wameunga mkono fikra zetu na wametuomba kwamba tuliharakishe.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe pale juu tutaona kuna maaskari wetu wa ulinzi, hawa wanatoka katika nchi za Afrika ya Mashariki, wanayo kawaida kuja hapa wakasalimiana nami, tukazungumza na wakauliza maswali mbali mbali yanayohusu Baraza. Mara hii waliniomba wangepata nafasi. Nikawaambia kwamba tutakuwa na bajeti ya serikali.

Kwa hivyo, nitamtuma Katibu hapa akawaambie kama wataweza wakasubiri mpaka kiasi saa 6:30 pengine nitaweza kuzungumza nao. Kwa hivyo, msione shida mkasema labda kuna uvamizi wowote, hapana. Ni maaskari wetu wanatulinda katika Afrika ya Mashariki, wanayokawaida wameshakuja kiasi mara mbili au tatu na mara hii wameona waje ili wanisalimie, lakini kimsingi imekuwa haiwezekani kwa sababu ya bajeti yetu. Lakini kama wataweza kustahamili naweza kuonana nao baadae.

Kwa bahati mbaya ni wengi kidogo, hata nafasi ya hapa ni finyu. Vinginevyo basi tungeweza hata kuwaambia wakatusikiliza hapa kinachoendelea, lakini nafasi yetu humu ndani ya ukumbi ni ndogo, kwa hivyo watakuwepo pale kwenye ukumbi mdogo wa juu.

Pengine kama kutakuwa na wale maafisa wakuu wa maeneo mbali mbali wawili au watatu wanaweza kuingia hapa, ili wakaweza kutuona tunaendelea na nini. Katibu unaweza kuifanya hivyo kazi. Mhe. Waziri endelea. Samahani nimekukatisha kidogo, niliona ni muhimu nitowe hiyo taarifa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakushukuru. Mhe. Spika, eneo jengine ambalo waheshimiwa wengi wameona walizungumze ili tuweze kulitolea ufafanuzi ni kuhusu mapitio ya bajeti kwa mwaka 2009/10 ambapo kidogo wengine walizungumza kwamba tumefikia hata kutoa *theme* nyengine mwaka huu, wakati ile ya mwaka jana hatukuweza kuifanyia tathmini. Nalo hilo waheshimiwa kadhaa walilizungumza, lakini nitatoa ufafanuzi wake na umuhimu wa kuwa na *theme* kila mwaka.

Suala la viwanda Mhe. Spika, nalo limechukua umuhimu wake kwamba viwanda vimekufa na serikali inachukua mwelekeo wa juhudi gani. suala hili limeguswa na wajumbe wengi na nimeona linamchango mkubwa katika kuchangia pato la taifa. Serikali imeona kuwa kuna juhudi maalum tuzifanye.

Pia kuna Waheshimiwa Wajumbe wengi wametushauri katika kutafuta vianzo vingi vya mapato. Hilo tunakubaliana nalo, kwamba sio kuwa tuzidishe nguvu kwa hivi vilivyopo tu, lakini wanashauri pia tujaribu vyengine. Hilo ndio suala la msingi kabisa ambapo baadae nitaelezea hasa huko tulikotoka tulikuwa vipi kibajeti na kimapato mpaka hii leo.

Mhe. Spika, mchango wa hospitali hasa hodi ya wazazi kwenye operesheni zile za *caesarean*. Nalo limejitokeza kwa nguvu sana hasa kwa ndugu zetu waheshimiwa wakina mama. Nitalitolea maelezo kidogo, lakini hasa tutawaachia wenyewe wakati sekta ya afya watakapokuja kulitolea ufafanuzi mrefu kabisa. Lakini kwa kweli *concern* yao sisi kama serikali tumesikia. Kuna ulazima wa kutupiwa jicho na kuweza kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, suala la kumi na moja ni suala la *JFC*. Hata Mhe. Fatma Fereji alipomalizia alilizungumza hilo, nalo nitalitolea maamuzi na hili nalo ni kweli niseme ni kidonda au ni kitu ambacho kinahitaji ufumbuzi. Kitu kikiwa pande mbili wewe utatimiza wajibu wako, lakini wewe cha kufanya itabidi umuhimize tu, huwezi kumvuta shati. Sasa tuna *role* kama hapo kumzungumza mwenzetu, kumsaidia na yeye au kumuhimiza. Lakini kama ninavyosema ni pande mbili. Kwa hivyo, hili suala lina ugumu wake kidogo. Sisi tumeshafanya jukumu letu na *role* yetu na tutazidi kuwahimiza wenzetu ili tulikamilishe kwa manufaa hasa ya upande wetu.

Pia kulikuwa kuna ushauri kwamba tuongeze nguvu kwa faida ya nchi wakati wa majadiliano. Mhe. Assaa, Mhe. Juma Duni na wengine walihisi labda kule tunapozungumza kwenye makero ya Muungano, labda tunaoneana haya kwa vile ni chama tawala. Sio kweli Mhe. Spika, kule tunazungumza kero tulizonazo na zinazotukabili na kule tunazungumza kwa ukweli, tunazungumza kwa uwazi. Maana yake hatutukanani, tunaambizana tu tena hakuna mwandishi wa habari hatutaki yatoke nje, yale ni yetu. Kwa hivyo, tusiwe na wasi wasi Mhe. Spika, tukija kuhitaji nguvu basi hakuna tatizo tutakuja tu, hee! bwana mheshimiwa Nassor na Mhe. Mohamed Ali Salim twenzetuni bwana kuna masuala ya elimu haya na tunafanya hivyo. Lakini kwa sasa naona wazungu wanasema *the ball is steal now in our control.* Naomba tuachieni kidogo, tutawashirikisha wakati wake ukifika.

Mhe. Spika, kwa ujumla haya ni mambo ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi na sasa naomba niwatambue waheshimiwa wote waliochangia hotuba hii. Kwanza kabisa ni:-

1. Mhe. Haji Omar Kheir Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti
2. Mhe. Said Ali Mbarouk
3. Mhe. Mkongwe Nassor Juma

4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Rashid Seif Suleiman
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Salmin Awadh Salmin
8. Mhe. Said Kheleif Ali
9. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
10. Mhe. Mhe. Haji Faki Shaali
11. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
12. Mhe. Juma Duni Haji
13. Mhe. Ali Abdalla Ali
14. Mhe. Mohamed Ali Salim
15. Mhe. Ali Denge Makame
16. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
17. Mhe. Zakiya Omar Juma
18. Mhe. Ame Mati Wadi
19. Mhe. Abass Juma Muhunzi
20. Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi
21. Mhe. Asaa Othman Hamad
22. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
23. Mhe. Muhiddin Moh'd Muhiddin
24. Mhe. Zahra Ali Hamad
25. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi
26. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman
27. Mhe. Asha Moh'd Hilal
28. Mhe. Haroun Ali Suleiman
29. Mhe. Ame Ussi Juma
30 Mhe. Najma Khalfan Juma
31. Mhe. Omar Ali Shehe
32. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji

Mhe. Spika, wote hawa walichangia hapa ukumbini na tunawashukuru sana. Kwa upande wa waliochangia kwa maandishi ni:-

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum na
Mhe. Ashura Abeid Faraji.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba tunawashukuru sana waheshimiwa wote waliopata nafasi ya kuchangia na ninaamini wengi zaidi wangependa, lakini muda ni mdogo.

Kwa haraka nataka nianze kwa Mwenyekiti wa Kamati za Wenyeviti. Kwa kweli tunamshukuru sana kwa michango yake mingi, kama nilivyosema michango mingi safari ni ya kuelekeza, kufanya hotuba yetu iwe bora zaidi

pamoja na utendaji wetu. Kwa hivyo, na yeye alijikita zaidi kwenye upande huo wa kutoa maelekezo pamoja na ushauri.

Kwa upande wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kudai stakabadhi. Mhe. Spika, tunachoweza kusema ni kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar katika kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wanatoa stakabadhi mara wanapofanya mauzo na wananchi wadai stakbadhi pale wanapofanya manunuuzi.

Bodi ya Mapato imeandaa mkakati maalum ambao ni endelevu wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara, kwa ujumla juu ya umuhimu wa kutoa stakabadhi. Kwa kuandaa semina mbali mbali na kuendesha vipindi vya elimu ya kodi kupitia televisheni, redio, usambazaji wa vipeperushi, majarida na kadhalika.

Aidha ndani ya mpango mkuu wa miaka mitano ya Bodi ya Mapato suala la elimu kwa walipakodi limepewa kipaumbele.

Mhe. Spika, kuhusu usajili wa wafanyabiasha pamoja na wakandarasi. Mhe. Mwenyekiti pia alizungumzia suala zima la wafanyabiashara pamoja na wakandarasi kuwa wasajiliwe.

Ninachotaka kusema ni kwamba kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazotoa leseni zikiwemo Manispaa na Halmashauri za Wilaya, zimekuwa zikitumia udhibitisho wa kulipa kodi kabla ya kutoa leseni, ili kuhakikisha kwamba wale wote wanaopata leseni pia wamesajiliwa katika kulipa kodi.

Aidha kwa kushirikiana na Mradi wa *SMOLE*, *ZRB* inakusudia kuanzisha utamaduni wa kutumia *Block Management System*, ili kuweza kuwajua na kuwasajili wafanyabiashara kwa mujibu wa maeneo waliopo.

Mhe. Spika, pia kulijitokeza mjadala mkubwa au ushauri mwingi sana katika suala zima la vibali vya kazi kwa baadhi ya wawekezaji kwamba labda walikuwa wakizuiliwa. Ninachotaka kusema ni kwamba mgeni aliyepewa kibali cha ukaazi, yaani *Class C* hapasi kupewa kibali cha Ukaazi cha *Class B*, kwa maana ya kuajiriwa.

Isipokuwa anapaswa kupewa *resident permit Class A*, kwa maana ya kuwekeza, kutoa ajira kwa wageni pamoja na raia, ili waweze kuongeza mapato kwa nchi na hii ndio Sera ya Uhamiaji kuhusu wageni na ajira nchini.

Sasa wengine wanakuwa na matatizo kwa sababu wanataka kwenda kinyume na huu utaratibu uliowekwa. Lakini tunajitahidi kuwaelimisha ili waweze kufahamu na vile vile maafisa wetu wa Uhamishi wawe *flexible* kwa mujibu wa

taratibu za nchi na wala wasiende kinyume na taratibu za nchi. Kwa sababu tunajua nchi yetu ni ndogo na nguvu kazi iliopo tunataka itumike vizuri na wala hatukatai watu wanaotaka kuja kutusaidia, muhimu wafuate taratibu zilizopo.

Mhe. Spika, eneo jengo ambalo Mhe. Mwenyekiti aligusia, alituomba sana tuharakishe katika kuwasilisha Mswada wa Sheria kwa ajili ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Tunakubali ushauri wake na kwa kupitia Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi tutachukua juhudi za makusudi, ili kuhakikisha kwamba suala hili linatekelezwa mapema iwezekanavyo, kwani serikali inatambua kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo utaharakisha maendeleo ya wananchi majimboni. Vile vile serikali itahakikisha kuwa inaweka misingi imara ya matumizi ya mfuko huo.

Pamoja na hayo nia yetu ni kwamba mashirikiano kati ya Mbunge na Mwakilishi miongoni mwa majimbo yetu ya Unguja na Pemba pia yaimarishwe zaidi, kwa ajili ya kufanyakazi kwa pamoja kwa manufaa ya jimbo.

Mhe. Spika, katika suala zima la kuongeza mishahara ya watumishi wa serikali pamoja na kufanya mapitio ya mishahara ya Vikosi vya SMZ. Kwa mwaka wa 2009/2010 marekebisho ya mfumo wa mishahara, serikali iliahidi kulifanyia kazi suala hili kwa mwaka huu, yaani mwaka uliopita. Serikali ililifanyiakazi suala hilo kwa wizara zote za serikali kulingana na uwezo wa serikali.

Marekebisho yameanza kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambayo tayari imeshaandaa mfumo wake mapema na kuanza kulipwa. Vile vile Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambapo nao tayari wameshatengezewa mambo yao kama tulivyomsikia Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wakati alipokuwa akitoa ufafanuzi.

Kwa kweli kulikuwa na matatizo kidogo kwenye mishahara ya walimu, lakini hayo si makubwa sana isipokuwa yatarekebishwa tu. Kwa sababu kweli nusu ya wafanyakazi wetu ni walimu na *figure* yao ni kubwa sana na ku-*deal* nayo kuna kazi. Kwa hivyo, tumejaribu kuwarekebisha wengi sana, isipokuwa yapo malalamiko madogo madogo kama alivyosema Mhe. Waziri jana tutajitahidi kuyaweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti, alimaliza kwa ombi maalum ya barabara ya Pale Kiongele, ili naye anialike kwa ajili ya kufurahi pamoja. Mhe. Spika, tunaomba kuahidi kwamba barabara ya Pale Kiongele ni miongoni mwa barabara ambazo zimo kwenye Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2010/2011, imetengewa jumla ya

shilingi 100 milioni kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo barabara hiyo na matengenezo yanatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mjumbe aanze kutafuta ng'ombe kabisa na baada ya kumaliza barabara ile basi tuchinje tule pilau kwa pamoja katika hali ya furaha *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye michango ya Mhe. Said Ali Mbarouk ambaye ni rafiki yangu. Kwanza kama nilivyosema ninamshukuru sana kwa hotuba yake ndefu na siku ile nilimtania kwa kumuuliza mbona ule ukili hukuja nao leo, alisema ameusahau tu. *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli tunamshukuru sana Mhe. Mjumbe, kwa sababu michango yake ilikuwa *very constructive* na nitajitahidi kugusa hapa na pale ambayo muhimu kwa yale aliyoyauliza.

Kuhusu utekelezaji wa Ilani ya CCM juu ya Kupunguza Umasikini na Kufanya Maisha yawe Bora kwa Mzanzibari, je MKUZA umesaidia kumuwezesha Mzanzibari kuwa na maisha bora. Ninachotaka kusema ni kwamba utekelezaji wa MKUZA unakwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya CCM, ambayo ni moja kati ya malengo yake makuu ni kufanya maisha bora ya Mzanzibari pamoja na Mtanzania kwa jumla.

Ripoti mbali mbali zikiwemo za utekelezaji kisekta na ule utekelezaji wa MKUZA zimeonesha kupiga hatua kubwa katika kufikia lengo hili. Katika kipindi cha utekelezaji wa MKUZA huduma za usambazaji umeme vijijini zimeimarika kwa kuweza kupatiwa huduma hii muhimu kwa maendeleo ya jamii.

Aidha huduma nyengine muhimu zilizoimarishwa ni pamoja na kilimo, ujenzi wa barabara, ujenzi wa bandari, kuongezeka idadi wa wanafunzi katika vyuo vikuu, mapambano dhidi ya malaria pamoja na upatikanaji wa maji safi na salama *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mafanikio haya ya utekelezaji wa MKUZA, ndio yamesaidia kwa mwananchi wetu kuendeleza shughuli zao mbali mbali za uzalishaji au kwa urahisi pamoja na ufanisi, ikiwemo biashara na viwanda vidogo vidogo. Kwa lengo la kujiongezea kipato na uwezo wao wa kununua na hatimaye kuweza kujiwekea akiba kwa maendeleo ya baadaye.

Kwa mfano, tuangalie leo unatoka Chake Chake na kwenda Micheweni, yaani mtandao ulivyokuwa mzuri wa barabara na gari zilizopo. Vile vile kutokea Mkoani na kuelekea Chake Chake labda tukumbuke barabara ilivyokuwa huko

nyuma na leo, boti imeshafika unakimbilia. Sasa haya yote yanarahisisha bidhaa kupelekwa na kupokelewa pamoja na wananchi wenyewe kufanyakazi zao.

Nadhani Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alielezea hapa kwamba si lengo la MKUZA kwamba tuchukue fedha tumtilie mtu mfukoni na kuweza kutumia aa! Isipokuwa sisi tunamuwezesha pamoja na kumrahisishia zile njia za uzalishaji, ili maisha yake wawe rahisi na hilo ndilo lengo letu.

Kushuka kwa mfumko wa bei nako kumeshababishwa na juhudi za uzalishaji wetu wa ndani, bali umetokana na kushuka kwa bei ya mchele na mafuta, ambapo Mhe. Mjumbe ali-*comment* hilo.

Mhe. Spika, sababu zilizochangia kushuka kwa mfumko wa bei si zile za nje tu, bali hata za ndani. Kwa upande wa sababu za ndani zilizochangia kushuka huko pamoja na hali nzuri ya hewa ambayo ilipelekea ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Chakula na vinywaji baridi bei zake zilipanda kwa asilimia 10 kwa mwaka 2009, zikilinganishwa na asilimia 24 kwa mwaka 2008.

Aidha bei za vyakula la vinywaji vina mchango mkubwa, asilimia 57.4 katika mfuko. Maelezo haya yanapatikana katika hotuba yangu kwenye ukurasa wa 50 ibara ya 54 na kitabu cha kwanza ukurasa 17 ibara ya 3.6. Vile vile ukurasa wa 12 kitabu cha kwanza kilieleza pia uzalishaji wa mpunga umeongezeka kwa asilimia 29 kwa mwaka 2009.

Nafikiri haya yote tuliyaona mwaka jana vipi mavuno ya mpunga yalivyokuwa mazuri kutokana na mvua ilivyokuwa nzuri na mategemeo yetu mwaka huu *Inshaallah* mpunga utakuwa mwingi *(Makofi)*.

Mhe. Mjumbe, pia alizungumzia juu ya suala zima kwamba bajeti yetu mwaka huu haikulenga kumuondolea mzigo wa unyonge na umasikini uliokithiri mwanamke hasa wa Kizanzibari. Kutokana na hali hiyo, alishauri mambo mengi tu kama vile sheria ya mfumo ibadilishwe, upendeleo wa kibajeti uwepo, kuanzishwa kwa madawati kijinsia, kuanzishwa kikundi kazi, kuongeza ushirika wa wanawake katika nafasi za uamuzi, kuanzishwe Kitengo cha Kutathmini. Kwa kweli alishauri mambo mengi sana na haya yote ni ya kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika isipokuwa ninachotaka kusema ni kwamba utayarishaji wa bajeti kwa kiasi fulani unazingatia jinsia, kwa kuwa maafisa wa bajeti na mipango wa Wizara ya Fedha na Uchumi wamepatiwa mafunzo maalum ya kuzingatia jinsia katika matayarisho ya bajeti.

Aidha miradi na *programs* za elimu, afya na maji nayo pia utekelezaji unasaudia katika kuimarisha masuala ya jinsia. *Programs* za uwezeshaji zinazotekelezwa na serikali kama vile Mifuko ya AK na JK, Mfuko wa Kujitegemea na kadhalika nayo pia inasaidia kuinua uwezo wa kiuchumi wa wanawake.

Vile vile mawizara pamoja na wilaya zetu zote zinazo madawati ya jinsia ambayo yanasaidia katika mazingatio ya jinsia katika sehemu hizo.

Kikundi kazi kimeanzishwa cha kushughulikia na kusimamia uzingatiaji wa kijinsia katika mipango, sera na sheria. Kwa kweli kinamama hatukuwaacha nyuma kabisa, yaani tumewaweka mbele na tunaamini kwamba uwezo wanao na wanaweza ku-*deliver (Makofi).*

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja nyengine kuhusu idadi ya wafanyakazi, ambayo haikufahamika vizuri au tuliiripoti vibaya. Hili Mhe. Mjumbe aliliona, Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui nao walilizungumza, kwamba wafanyakazi wapatao 5,943 ninashukiwa kuwa ni wafanyakazi hewa, ambapo serikali haijui wafanyakazi wangapi na pengine kupokea mishahara hewa. Kuhusu tofauti za tarakimu za ajira baina ya Hotuba ya Serikali na kitabu cha kwanza.

Kwa ufafanuzi Mhe. Spika, idadi halisi ya waajiriwa ni 5,943 ni ongezeko la waajiriwa lililojitokeza kwa mwaka 2009, ambapo kulikuwa na waajiriwa 47,551. Idadi hii ni sawa na asilimia 14.2 ikilinganishwa na idadi ya waajiriwa kwa mwaka 2008 waliokuwa 41,608. Mchanganuo uliotolewa ulihusisha takwimu za mwaka 2008 na sio mwaka 2009, yaani hapo ndipo kidogo palipokuwa na *confusion*.

Mchanganuo kwa mwaka 2009 ni kama ifuatavyo:-

1. Sekta ya Umma ni 35,724 na
2. Sekta Binafsi ni 11,827

Kwa hivyo, napenda kumdhibitishia Mhe. Mjumbe kwamba hakuna mfanyakazi hewa.

Aidha kuhusu tofauti za tarakimu zilizotumika katika kitabu cha kwanza, tunakiri kwamba tulitumia takwimu za awali, ambapo hatukufanya marekebisho kwenye kitabu cha kwanza baada ya kupatikana takwimu za mwisho ambazo ndizo za uhakika. Kwa hivyo, nakubali kwamba kosa hilo limepelekea kupotosha dhana nzima. Mhe. Spika, tunaomba radhi kwa hilo.

Mhe. Spika, kulikuwa na ombi la kupunguza kiwango cha kodi la Ongezeko la Thamani (*VAT*) hadi kufikia asilimia 5, Mhe. Mjumbe aliuliza hili pamoja na waheshimiwa wengine.

Kupunguza kiwango cha utozaji wa kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kutoka asilimia 18 hadi 15, kunahitaji kufanyiwa tathmini ya kina, ili kuweza kujua ni kiasi gani cha mapato ya serikali itapoteza, jinsi gani pengo litalotokana na asilimia 3 itakayopunguzwa litaweza kuzibwa.

Kwa kweli hilo linawezekana, lakini naomba mtupe nafasi kwa ajili ya kulifanyia utafiti na tathmini nzima na halafu tutaweza kutoa kauli kwamba tupunguze kama walioko chini ya hapo.

Mhe. Spika, kutokana na misaada ya kibajeti ya 4.5, Zanzibar tuliambiwa imepata alivyosema Mhe. Mjumbe kwamba ilipata shilingi 50 bilioni katika mwaka 2009/2010 kama *style* yake. Kwa mujibu wa Bajeti ya SMT aliendelea kusema kwamba jumla ya shilingi 2,379.559 zilizolewa na washirika wa Maendeleo kama *GBS* kwa Tanzania, fedha hizo ni sawa na shilingi 107 bilioni ambazo ni stahili ya SMZ.

Naomba kuweka sawa hili kidogo na hata Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alililiuliza. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba naomba nukuu aliyoichukua Mhe. Mjumbe labda hakuipata vizuri.

Kwa sababu katika ibara ya 22 ya Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano inaeleza kwamba fungu la *Budget Suppor*t, misaada pamoja na mikopo ya Kibajeti zilipatikana jumla ya shilingi 2,379.559 milioni, ambapo asilimia 4.5 ya kima hiki ni shilingi 107 bilioni na wala sio 50 bilioni tulizopewa kama ilivyoripotiwa.

Mhe. Spika, naomba kulieleza Baraza lako kuhusiana na utata huu, kwamba ile nukuu hasa hivi ndivyo ilivyo kama kulikuwa na *distortion* kidogo ambayo Mhe. Mjumbe hakuipata, basi *data* hizi tunaweza kumpa baadaye. Lakini hii niliyoisoma ndiyo nukuu hasa alivyolizungumza Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimnukuu Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi wa SMT alichosoma kwenye ibara ya 22 ya hotuba yake.

> Kwenye kitabu cha Hotuba ya Mpango wa Maendeleo wa SMT ibara ya 22 inasema hivi:-

> "Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010 jumla ya misaada ya na mikopo ya kibajeti (*GBS*) iliyopokewa ilikuwa shilingi 998.676 bilioni sawa na asilimia 84 ya shilingi 1193.91 bilioni zilizokadiriwa kwenye bajeti, nafikiri hata Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alisoma hili.
>
> Misaada na mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikijumuisha Mfuko wa *Basket* ulifikia shilingi 1380.883 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio katika kipindi hicho".

Sasa hiyo ndiyo nukuu ambayo nilitaka kuinukuu, ili Mhe. Mjumbe aone kidogo labda yeye hakuinukuu vizuri.

Maana yake nini. Mhe. Spika, kutokana na nukuu hizo utaona kuwa tarakimu alizotoa Mhe. Mjumbe si sahihi na kwamba kidogo hakuzifanyia uchambuzi wa kina. Hata hivyo, nataka kusema kwamba kutokana na tarakimu alizotoa Mhe. Waziri wa Fedha wa SMT kwa misaada ya kibajeti Zanzibar iwe na makisio ya shilingi 53.73 bilioni, ambazo sisi tulifikia shilingi 50.114 bilioni na tulitakiwa tupate shilingi 53.73 bilioni, kwa hiyo tulipokea shilingi 50.114 bilioni.

Aidha tulitakiwa kupokea shilingi 44.94 bilioni, lakini tumepokea shilingi 40.93 bilioni mpaka Machi, hadi mwezi Juni tumepokea jumla ya shilingi 51.218 bilioni.

Kwa kweli hili si tatizo kwa vile huwa tunafanya masawazisho na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania hapo baadaye, yaani ikiwa kuna kasoro basi tunafanya masawazisho na wala hatugombani. Kwa sababu hizi *figure* zote hao wafadhili wanatoa na kuweka hesabu zao na sisi tunaweka zetu.

Kwa hivyo, tunazifanya mpaka tuone mpaka zimeoana na maafisa wetu wanakwenda na kukaa pamoja wa *External Finance* mpaka tunafikia maamuzi, yaani hapa hawatunyimi na tunashukuru kabisa kwamba tunakwenda vizuri. Kwa upande wa lile gawio letu la 4.5, basi ndio tunapatiwa hicho.

Mhe. Spika, nadhani nimejitahidi sana kutoa ufafanuzi kuhusu hoja za Mhe. Mjumbe, lakini kulikuwa na hoja moja ambayo hata Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Mhe. Makame Shimba Mbarouk pamoja na wengine walizungumza kuhusu suala la Mkurugenzi wa Vitabumbulisho, kwamba imetenga jumla ya shilingi 243 bilioni kwa matumizi ya takrima.
Wakati Idara ya Sekondari ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imetengewa jumla shilingi 160 milioni na Idara ya Kinga shilingi 150 milioni

na Vikosi vya SMZ shilingi 25 bilioni na Kamisheni ya Utalii ni shilingi 737 milioni.

Mhe. Spika, ukifungua lile buku letu la mahesabu yote Fungu 23,000 linahusiana na takrima na uendeshaji kazi ambayo ina kasma mbili. Kasma ya kwanza namba 23,000 na 4 inayohusiana na matumizi ya takrima ambayo imepangwa kutumia shilingi milioni 1 tu kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Vitambulisho amepangiwa kutumia takrima shilingi milioni 1 tu kwa mwaka. Kifungu namba 2 kasma namba 23,000 na 5 inahusiana na matumizi ya *General Expenditure* au matumizi mengineyo kwa jumla, ambayo yamepangiwa shilingi 242 milioni na laki 9 kwa mwaka, hivyo jumla ya fungu ni shilingi 243 milioni na laki 9.

Kwa hivyo, matumizi halisi ya takrima yamepangwa kutumia jumla ya shilingi milioni 1 tu kwa Unguja na Pemba kwa mwaka mzima, ambayo ni sawa na shilingi 84,000 kwa mwezi au shilingi 4,115 kwa siku badala ya shilingi milioni 1 ambazo pengine waheshimiwa wame-*misquote*. Nadhani ni vyema kutoa ufafanuzi wa *correct interpretation* wa hizi hesabu, labda kidogo hazikukaa sawa na tunaomba radhi kwa hilo. Lakini hii ndiyo tuichukulie hesabu halisi kabisa.

Mhe. Spika, nikiendelea na kutoa ufafanuzi naomba nizungumze kwa jumla kwa waheshimiwa wengine waliochangia. Kwa kweli kama nilivyosema kwamba hoja zilikuwa nyingi na hesabu inavyoonesha kwamba waheshimiwa nao wametusaidia sana kwa michango yao mizuri kabisa.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mhe. Mkongwe Nassor Juma, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Mohammed Ali Salim, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Abass Juma Muhunzi, Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, Mhe. Assaa Othman Hamad, Mhe. Suleiman Hemed Khamis na Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin.

Kwa kweli wao walizungumzia sana kuhusu suala la kilimo, kwa kweli walikuwa na ari ya kutuelekeza, kutukosoa pamoja na kutaka kilimo kiende mbele. Nadhani wenyewe sekta ya kilimo itakapofika watatoa ufafanuzi kuhusu masuala ya kitaalamu ambayo mlitaka tuyaeleze.

Mhe. Spika, tunaposema Sekta ya Kilimo imeongeza hii tunaangalia hali ya uzalishaji ilivyokuwa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Katika mwaka 2009 kulikuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya chakula kwa asilimia

14 ikilinganishwa na mwaka 2008. Mazao yaliyochangia zaidi katika ukuaji wa sekta hii ni kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi, mpunga, muhogo, viazi vitamu, mbaazi na kadhalika. Kwa kuangalia hali halisi hiyo kwamba hayo ndiyo mazao makuu ambayo yana uzito kwenye sekta ya kilimo na biashara nchini mwetu *(Makofi)*.

Uanzishwajiwa wa Skuli za Wakulima, nao pia umesaidia sana kuwapatia wakulima wetu taaluma kwa wakati mmoja na kupelekea kuongezeka kwa uzalishaji.

Aidha uimarishaji wa miundombinu ya umwagiliaji na upatikanaji wa matrekta nao pia umesaidia kuongeza uzalishaji hasa mpunga.

Kwa upande wa utoaji wa vifaa vya uvuvi vile vile umesaidia kuongezeka upatikanaji wa samaki na kupunguza uvuvi haramu. Lakini kama tunavyojua wavuvi wetu hizo mashine wanazotumainia bado haziwafikishi huko tulikokusudia, yaani *deep see* kwa ajili ya kupata samaki wengi zaidi.

Mhe. Spika, serikali inaendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo. Hata hivyo, kulingana na mahitaji ya sekta nyengine na uwezo wa serikali kuu nguvu pia zimeelekezwa katika kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya barabara ambayo ni chachu ya maendeleo ya kilimo.

Vile vile serikali imekuwa ikizingatia na kuyapa umuhimu mkubwa mazao ya karafuu na mwani. Katika bajeti ya mwaka 2010/2011 kuna ongezeko zaidi ya asilimia 30 ikilinganishwa na mwaka 2009/2010. Hata hivyo, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira hupokea fedha kutoka Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza zao la karafuu.

Kwa upande wa uzalishaji wa mwani, si sahihi kama imeekewa vikwazo. Isipokuwa kinachofanyika hivi sasa ni majaribio ya uzalishaji wa mwani wa aina ya *Cottone*, ambao uzalishaji huo unaonesha unastawi vizuri kwenye kina cha maji mengi.

Aidha aina hii ya mwani ndiyo yenye bei nzuri katika Soko la Dunia ikilinganishwa na ile aina inayozalishwa kwenye kina kidogo cha maji. Mhe. Spika, tunaposema maji hatukusudii mtu aende *deep see* aa! Kwa sababu kule huo mwani utaupanda vipi. Kwa kweli ni maji mengi kulinganisha na ule mwani mwengine ambao uzalishaji wake kwenye maji kidogo. Sasa huu ndio ushauri wa kitaalamu.

Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi nao tuliulizwa kwamba hatukuipa kipaumbele, yaani hata fedha za ujenzi wa bandari na Kituo cha Usindikaji wa Samaki

zimerudishwa kwa kukosekana ardhi ya ujenzi. Mhe. Spika, nataka kusema kwamba Sekta ya Uvuvi inaendelea kupewa kipaumbele kutokana na umuhimu wake, yaani kiuchumi na kijamii. Kwa sababu kulikuwa na mipango ya ujenzi wa bandari na Kituo cha Usindikaji wa Samaki.

Hata hivyo, fedha hizo kwa upande wa Wizara ya Fedha na Uchumi hazijawahi kupokelewa. Kwa hivyo, tutazungumza na wenzetu wa Sekta ya Uvuvi au Wizara ya Kilimo kuona kwamba hiki kitu kipo tuweze kufuatilia na kuweza kuzipata hizo fedha na kuzitumia ipasavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba waheshimiwa ni wengi sana na hasa walizungumza suala la kwamba bajeti iongezwe uzalishaji mdogo. Kwa kweli hayo ni kama kutupa hamasa sisi kama wizara na serikali kwa jumla.

Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba sekta husika wakati watakapoleta bajeti yao, basi haya yote ambayo waheshimiwa mmeuliza au kutoa michango yetu watayagusia au watayatolea ufafanuzi. Kwa mfano, athari ya wadudu wa embe pamoja na mambo mengine mbali mbali, sasa nikiyachambua moja moja itakuwa naelezea Bajeti ya Wizara ya Kilimo na muda utakuwa mkubwa zaidi.

Lakini Mhe. Mkongwe Nassor Juma, Mhe. Said Khelef Ali, Mhe. Abubakar Khamis Bakary na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui walizungumzia juu ya suala zima la mbegu bora. Mbegu zinazotolewa kwa ajili ya kilimo cha juu hazistahamili na vile vivutio vilivyotolewa havisaidii wakulima wadogo wadogo, badala yake tuangalie zaidi kwenye mbolea, majembe ya ng'ombe na kadhalika. Vile vile walishauri kwamba vivutio vitolewe kwenye maeneo ya biashara na viwanda ambavyo vimedharauliwa. Hatukuvidharau lakini tuchukulie kwamba haya tumeshayazungumza huko nyuma.

Mhe, Spika, kwa mujibu wa jaduweli ya pili ya kodi ya ongezeko la thamani vifaa, mashine na huduma za kilimo na mifugo zilizosamehewa kodi ni pamoja na mbolea, dawa za wadudu waharibifu, dawa za kuulia magugu, dawa za kufukiza, dawa za kukuzia mimea, matrekta ya kilimo, majembe yake na majembe ya kuburugia na kulima, mashoka, mashine za kupandia na kusambaza mbolea, mashine za kunyunyizia dawa mashambani. Aidha kwa upande wa mazao ya kilimo matunda, vitunguu, mihogo, viazi, mboga mboga mahindi na nafaka nyengine, unga unatokana na nafaka, karafuu njugu na mbegu za miwa zimesamehewa kodi ya ongezeko la thamani Hii yote inalenga kumrahisishia mkulima wetu aweze kuzalisha kwa faida na hili sio geni. Wenzetu huko nje wanafika hadi mpaka wanakwambia usilime mwaka huu nitakupa fedha, sasa sisi hatujafikia uwezo huo kwa sababu bado *production* yetu ndogo kwa hivyo tunajikita zaidi kwa kuwaondoshea mzigo wa kodi katika hizi *input* za kilimo.

Kwa hivyo waheshimiwa naomba kuwajulisha tu kwamba hatukusahau na kama nilivyosema kwenye kipengele hichi cha jaduweli ya pili basi zote hizi zimeonyeshwa, tunapozungumzia zana za kilimo hatuzungumzii kwamba *ma-combine na harvester* kama nilivyosema matrekta na majembe yake, kuna vipawa tila vile vyote hivi tumewarahisishia ili wakulima wetu wadogo wadogo waweze kuviingiza.

Mhe. Spika, tunapozungumza uzalishaji sio lazima uwe na eka mia au mia na hamsini ile wenyewe wanaita e*xtensive agriculture* lakini *extensive agriculture* eneo dogo tu ya robo moja ya eka unaweza kuzalisha gunia ishirini za mpunga pale, hayo yanafanyika muhimu *input* zake zipatikane kwa mfano katika mpunga *input* kubwa ni maji wewe ukiyaweza maji na mbegu yako nzuri na mbolea ukatia wadudu ukawafukuza utapata mpunga na yanafanyika, wapo watu tayari wanamaliza msimu huu wanaanza msimu mwengine hawanunui mchele tunao wakulima kama hao huu mchele tunaonunua kutoka Thailand huko au Filipin hawazalishi kwenye maeneo makubwa, wanazalisha kwenye viploti vidogo vidogo tu lakini muhimu ni ile *extensive agriculture* na *input* zote nilizozitaja zinafanyika.

Sasa mambo haya ya msingi ndio tunayotaka na sisi tuyalete kwetu Kwapweza, Mtwango, Bahanasa kule kote huko Mhe. Assaa mabonde yako ya Msaani na Pujini tunataka maji tuyahifadhi halafu tutie mbolea utapata gunia ishirini na hununui mpunga tena.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo kwa upande wa kilimo nataka nilisisitize kwamba kwa lengo la kuhamasisha na kushajihisha na kuimarisha kilimo na ufugaji nchini, serikali imeongeza wigo wa msamaha katika kilimo na ufugaji kwa vifaa, mashine za huduma za kilimo kwa kusamehe na kutoa kodi ya VAT katika kuimarisha miundo mbinu ya umwagiliaji maji, ujenzi wa mabanda au mahema ya kuatikia na kulelea miche. Hatuzungumzii vibanda vya makuti tunakusudia kuna *green houses* na wapo.

Wilaya ya Kati kuna mkulima mmoja mzuri tu labda Mhe. Spika, baadae ikifika sekta ya kilimo ningemshauri tupate kidogo *study tours* tukamtembelee huyo mkulima aliyekuwa navyo vitu hivi inafurahisha sana, haya yanafanyika Zanzibar wapo hao watu tulifanya *business council* pale alialikwa yule mkulima akaja akaelezea mwenyewe hasa vipi anavyofanya? Sote tumefurahika tukauliza yanatendeka kwetu haya. Kwa hivyo sio vibanda vya makuti tayari watu wapo hapa kwetu sasa tuwasaidie na wao wakae hapa.

Kwa hivyo serikali ina imani kwamba misamaha hii itawasaidia wakulima wetu hata mkulima mdogo mdogo na kuongeza uzalishaji.

Mhe. Spika, kwa upande wa mbegu za mpunga wa juu mbegu hizi zimeanza kutolewa kwa wakulima mwaka 2009 kwa lengo la uzalishaji, aidha Wizara husika inaendelea na juhudi za kuizalisha kwa wingi ili wakulima wengi zaidi waweze kufaidika nazo.

Mhe. Mkongwe Nassor Juma alizungumzia suala la Gadava kwa Chuo cha Mbweni alisema kiitwe Gadava, hili neno ni la kitaalam sana na nimezungumza na wataalam wetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wametueleza kwamba kwa hivi sasa wanafunzi wanatumia *technology* mpya katika mafunzo ya afya ya binaadam aliyehai na mafunzo haya yanatumiwa kwa *X-ray na City scan* na wanajifunza *anatomic* kwenye kompyuta au CD na compyuta za DVD badala ya Gadava. Maana huyu Gadava humchukua yule mtu mwenyewe umchane kidogo wanasema hiyo ni *old technology* sasa vifaa kama hivyo vya *X-ray na City scan* unamuweka tu pale picha yote inamuonyesha pale, ndio maana zamani tulikuwa tunaogopa maiti akifa tu tunakwenda kumchukua siku ile ile unaogopa asije kupasuliwa akatolewa jicho, ubongo kwa kusomeshea hayo ndio ya Gadava anayosema Mhe. Mkongwe tumeshavuka huko sasa hatuko tena. Kwa hivyo Mhe. Bimkongwe tunakushukuru kwa hayo uliyoyapata huko lakini tumeshavuka huko.

Mhe. Spika: Hivi gadava ni *skelaton* au?.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Ndio Mhe. Spika ni kama skelaton au maiti hasa.

Mhe. Spika, bei za fidia ni ngogo na miti tumeambiwa kwamba inapotolewa wakabidhiwe wenyewe tumeshauriwa tu, Mhe. Mkongwe Nassor Juma aliuliza hilo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliuliza, Mhe. Said Khelef Ali nae pia aliuliza ukweli ni kwamba fidia ya mazao inayotolewa haikidhi haja hilo tunakubali, kweli kabisa bei tulizokuwa nazo zimeshapitwa na wakati. Kwa hivyo serikali inafanya mapitio ya fidia ya mazao kwa lengo la kuweka viwango vipya vinavyokwenda na wakati.

Mhe. Spika, suala la uchimbaji wa mafuta hili nalo limezungumzwa na Waheshimiwa wengi sana wanatuuliza tumefikia wapi waziri atoe maelezo ya kina hakuna mgao wa fedha, sio suala la kutafuta hayo mafuta yanachemka tu yapo majani yanaungua mpaka lini tunayakalia. Waheshimiwa wengi sana hilo wamelizungumza takriban wote sina haja hata ya kuwataja majina kwa sababu imeonekana kama serikali inachelewa baada ya maamuzi ya baraza, ninachotaka kusema Mhe. Spika, ni kwamba naomba niwatoe waheshimiwa wasi wasi kama wanao kwa kuulizia hatua iliyofikiwa kwa suala hili.

Wasi wasi huu umetokana na kwamba sikusema kama nilivyosema hapo mwanzo kwamba sikutoa maelezo kwamba tumefikia wapi? L akini naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Tafana Kassim Mzee Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa maelezo aliyoyatoa, kama alivyoeleza juhudi mbali mbali za matayarisho zinaendelea. Hapa zaidi tunajikita kwenye mtayarisho hili suala naomba kulizungumzia sana tunajikita kwenye matayarisho, miongoni mwa hatua za matayarisho ni zile za kujenga uwezo ambapo zoezi la kutafuta vijana wa kupelekwa kwenye masomo ya juu zinaendelea, aidha marekebisho ya sheria mbali mbali yatahitajika ambapo itabidi turekebishe sheria kama alivyozungumza Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Kwa hivyo Wizara ya MUNA tayari inalifanyia kazi suala hili suala hili la utafutaji wa mafuta na uchimbaji wake hususan baharini sio la muda mfupi ni la muda mrefu na hivyo linahitaji ustahamilivu na mipango mizuri kabisa, juzi tulikuwa na semina baada ya kukosa ile dozi waliyotupa hapa wale wenzetu wa Norway kwa upande wa Mawaziri basi tukaomba watufanyie na yetu sisi. Wametushauri sana na wametwambia kwamba ni bora kuchelewa lakini matayarisho yawe mazuri kwa sababu gani kweli wanasema kuwa na mafuta ni barka lakini yanaweza kuwa balaa na balaa yenyewe kwa hii nchi yetu sio kwamba tutapigana wenyewe aa, lakini kwa hii nchi yetu tukikosea zile *step* zake basi inaweza kuwa kero tunaweza kuchafua nchi yetu maliaisli yote ikachafuka na huo utajiri wenyewe tusiupate.

Sasa wametushauri kwamba tuende hatua baada ya hatua na wao wamesema mfano huo Wanorway wamechiua miaka kumi tokea ku- *explore mpaka ku-extract* wakaanza kuuza *commercial* miaka kumi, sasa wametushauri sana kwamba jitahidi sana mwende step kwa step hatutaki kuulaza lakini twende hatua kwa hatua ni muhimu sana, hilo wametushauri san asana na wao wameyaona kwamba yanachemsha. Lakini huo ndio ushauri wao na sisi tumelichukua lakini Wizara itakapokuja wenyewe watalielezea kwa urefu zaidi zile hatua ambazo wamejitayarisha nazo.

Mhe. Spika, suala la uzalishaji viwandani nalo lilizungumzwa sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Rashid Seif Suleiman , Mhe. Hijja Hassan Hijja, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Abas Juma Mhunzi na wengi sana wamelizungumza suala hali na wameelezea hasa uzoefu wao wa miaka ya nyuma na mpka hapo tulipofikia hii leo. Nataka kusema yamejitokeza mafanikio tofauti katika maeneo ya uchumi yaliyowekeza mkazo katika dira ya maendeleo ya 2020, wakati mafanikio ya kuridhisha yamepatikana katika maendeleo ya utalii na uzalishaji wa viwandani bado haukupiga hatua tunakiri hakupiga hatua kubwa katika nusu ya kwanza ya kipinchi cha 2020.

Hivyo basi tutalazimika kuweka nguvu katika nusu ya pili inayoanza mwakani ili mafanikio yapatikane katika eneo hili serikali itaangalia kwa kina mambo yanayoathiri viwanda na kuchukua hatua mahususi zikiwemo za kutoa vivutio maalum, mkakati wa kuimarisha viwanda utaunganishwa na hatua maalum za kuimarisha ajira kwa vijana wanawake na wawekezaji wazalendo kwa kuzingatia sera ya maendeleo ya viwanda kwa sasa inafanyiwa mapitio, mkakati wa usafirishaji nje pia umeandaliwa, utafiti wa *valley chain* umefanyika kwa msaada wa shirika la Umoja wa Maendeleo la viwanda la umoja wa mataifa yaani UNIDO. Aidha changamoto kubwa ni utekelezaji katika mapendekezo yaliyomo katika utafiti huo na mikakati iliyotajwa.

Mhe. Spika, serikali imeweka msisitizo maalum katika kushajihisha na kuunga mkono juhudi za wawekezaji binafsi nchini, viwanda tunashajihisha wawekezaji ndio waweke serikali huko tena haijishuhulishi na hayo tena, ila tunaweka sera nzuri tu ili wawekezaji waje wawekeze. Mmetwambia matatizo madogo madogo yaliyojitokeza hayo tutayafanyia kazi kama uhamiaji na mengine, lakini serikali hatuko tena huko mfano wa viwanda vya mafuta ya nazi, viwanda vya nguo huko sasa waende watu binafsi sio serikali tena.

Tokea mwaka 2004 sera mpya ya uwekezaji iliandaliwa na kufuatiwa na sheria mpya iliyochukua nafasi ya sheria tatu zilizokuwa zikitumika awali kwa ajili ya wawekezaji nchini chini ya ZIPA. Kwanza kulikuwa na mamlaka ya maeneo huyu ya uchumi na iliyokuwa mamlaka ya Bandari huru, taasisi hizo ziliunganishwa na kuundwa mamlaka moja tu ZIPA ili kuongeza ufanisi, wakati mafanikio yamepatikana katika uwekezaji na kwenye utalii kasi ya uwekezaji katika maeneo huru ya Fumba na Micheweni bado ni ndgo nakubali, kamati wanasema walitembelea na hiyo tunakubali kwamba kazi ya uwekezaji katika maeneo huru ya Fumba na Micheweni bado ni ndogo kinyume na juhudi zilizochukuliwa na serikali za kuyatangaza kwa wawekezaji.

Serikali itandelea kuyatangaza maeneo haya ushauri wa waheshimiwa wawakilishi juu ya kuimarisha na kuyalinda maeneo haya yasivamiwe utazingatiwa na utachukuliwa hatua ipasavyo.

Kwa upande wa eneo la Fumba kukamilika kwa barabara ya Mazizini/Fumba tunaamini utasaidia sana kuendeleza kwa upande mmoja. Aidha serikali kwa mwaka ujao wa fedha inakusudia kuanza ujenzi wa barabara inayopitia maeneo hayo ya Fumba yaani *ring road* ile kwa kutoa shilingi bilioni mbili kwa kuanza kazi za ujenzi, zimeshatengwa bilioni mbili kwa ujenzi ule wa *ring road* inayokwenda Fumba.

Mhe. Spika, suala la uwezeshaji kwa wananchi kupitia mifuko ya JK na AK uharakishwe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Ali Abdalla Ali na waheshimiwa wengine hili walilizungumzia sana na tunakubali ushauri wao, lakini ninachotaka kusema tu pamoja na ushauri hasa Mhe. Ame Mati kwa Matemwe kule ujitahidi ufuate taratibu zilizowekwa wewe usaidie ku- *facilitate* nakumbuka bajeti iliyopita ulizozana kidogo na Mhe. Asha kwamba hujapata hata mtu mmoja kwako. Tatizo lenyewe ni zile taratibu tu basi wewe ukizifuata zile taratibu hakuna tatizo lolote.

Mhe. Salmin Awadha Salmin na yeye alisema jimboni kwake Magomeni hata mtu mmoja hajapata sasa tujiulize kwa nini kama wengine wanapata wewe hujapata kuna tatizo gani? Basi ukilifanyia kazi hilo hakuna tatizo lolote hizo zimewekwa kwa watu wote. Kwa hivyo mfuko wa uwezeshaji kwa wananchi wa JK na AK umepanga kutoa jumla ya shilingi bilioni tatu nukta sita, ambapo kwa Pemba shilingi bilioni moja nukta mbili na kwa Unguja shilingi bilioni mbili nukta nne. Mgawanyo huu umezingatia idadi ya wakaazi hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi ambao umetengewa jumla ya Shilingi bilioni moja nukta mbili ambapo kila mkoa ulipangiwa shilingi 0.6 bilioni.

Mhe. Spika, hadi tarehe 31 Machi, mwaka huu jumla ya shilingi bilioni 1.28 zimeshatolewa kwa wananchi na vikundi vya wajasilia mali na vikundi vya kuweka na kukopa yaani SACCOS, kati ya fedha hizo Unguja zimetolewa shilingi milioni 883 sawa na asilimia 69 na Pemba zimetolewa shilingi milioni 399 sawa na asilimia 31. Ijapokuwa kuna mafanikio ya utoaji wa mikopo hiyo bado kuna baadhi ya sheria ziko nyuma kupata mikopo kutokana na baadhi ya wananchi kutofuata taratibu na kutotoa taarifa sahihi za miradi yao kama nilivyosema, hata hivyo serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kufanikisha lile lengo lililokusudiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Rashid Seif Suleiman walitaka maelezo zaidi juu ya mishahara ya wafanyakazi kwamba bado iko chini wakati gharama za maisha ziko juu, ukweli ni kwamba kwa mwaka 2010/2011 serikali imekadiria kutumia shilingi 82,459 milioni ambapo pato la taifa linatarajiwa kufikia shilingi bilioni 878.4 kwa bei za mwaka husika, hivyo mishahara inategemewa kufika asilimia 9.4 tu ya pato la taifa kinyume na asilimia hamsini ambayo imeelezwa. Kwanago hiki ni kidogo ikilinganishwa na asilimi ishirini iliyotajwa kwa nchi kama Afrika ya Kusini n.k.

Kuhusu ongezeko dogo la wastaafu serikali itachukua hatua ya kuongeza kadiri hali itakaavyoruhusu, tuanze kidogo kidogo tuende na nashukuru baadhi ya waheshimiwa wamekubali juhudi zetu kwamba tuongeze kadiri hali inavyoruhusu.

Suala la gesi kwamba serikali imeshindwa kutatua tatizo la kiuchumi hili nalo mgao wa 4.5 vigezo vinavyotumika SMZ itapataje taarifa za misaada yote inayopata Tanzania, mambo mengi sana haya waheshimiwa wameyauliza na takriban weheshimiwa wengi sana waliochangia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Abubakary Khamis Bakari, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Nassor Ahmed Mazurui, Mhe. Mohammed Ali Salim, Mhe. Zakia Omar Juma, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Assa Othman Hamad, Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi na wengi wengine walichangia na kuulizia suala hili.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba hili ni eneo muhimu sana katika mstakbali wa Zanzibar ndani ya Muungano na ndio maana nikalitolea maelezo maalum katika hotuba yangu, kama waheshimiwa wawakilishi walivyoeleza ufumbuzi wa matatizo mbali mbali umechelewa kupatikana hilo tunakiri. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji ametuuliza kila mara na kila mwaka imekuwa nyimbo tu tunakiri kwamba ufumbuzi wake umechelewa kupatikana, hata hivyo serikali zetu mbili zinaendelea kutafuta suluhu ya masuala haya. Najua na kama nilivyosema mapema unapodili na mtu mwengine hata wewe mwenyewe kitu chako mwenyewe tu kama maamuzi basi unaamua tu, lakini sasa kama una mwenzio katika maamuzi lazima mridhiane lakini usilale ukangoja mpaka atakapokuwa tayari yeye. Hilo tunakubali tutajitahidi kulisukuma tupate mafanikio kwa upande wetu.

Kuhusu vigezo vilivyotumika kupata mgao wa asilimi 4.5 kiwango hiki kinatokana na mapendekezo ya mpito *entery management* ya Shirika la Fedha Duniani IMF awali kiwango hicho kilipendekezwa kwa mgao wa gawio la faida ya Benki Kuu tu peke yake, lakini baadae ikakubalika pia kitumike kwa misaada ya kibajeti ilishauriwa kigango hicho kiwe cha muda tu wakati serikali mbili zikitafuta kiwango cha kudumu. Vigezo vikuu vilivyotumiwa na IMF ni pamoja na idadi ya watu mzunguko wa fedha baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pato la taifa, kwa wakati huo kiwango cha chini kilipaswa kuwa aslimia tatu na cha juu asilimia sita hayo ndio mapendekezo. IMF ilipendekeza kiwango cha asilimia 4.5.

Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu mtizamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa mgao wake ulipaswa kuzingatia hisa zake wakati wa kuanzishwa kwa Benki kuu na sio vigezo vilivyotumiwa na IMF, kigezo hicho kikitumika basi SMZ itastahiki asilimia 11.052 ya gawio la fedha za benki kuu.

Mhe. Spika, kuhusu uwezo wa SMZ kukopa ndani SMZ haihitaji kupitia Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukopa, badala yake inakopa moja kwa moja kupitia minada ya hati fungate na

dhamana za serikali inayosimamiwa na benki kuu, wao benki kuu wanasimamia tu kwa hivyo tunakopa moja kwa moja kwao.

Kuhusu mikopo ya nje hili ni moja ya makubaliano ya muungano ni suala la muungano na hivyo dhamana yake kuwa chini ya Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mikopo inayohitaji dhamana ya serikali, lazima SMT itu- *guarantee* kwa ile mikopo ya nje lakini hii ya ndani hatuhitaji kupita kwao. Hili sio la leo ni la muda mrefu kabisa nimekwenda kuitafuta bajeti ya mwaka 2000 ya hotuba ya serikali naomba nikariri kuthibitisha hili kwamba lipo zamani.

" Ukurasa wa 56 paragraph 97 inasema Mhe. Spika, hivi karibuni makubaliano yamefikiwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwezesha SMZ kuwa na mawasiliano moja kwa moja na wafadhili na nchi rafiki kuhusu misaada ya nje".

Sasa tafsiri ya uamuzi huo ni kuwa hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua jukumu lote la utafutaji wa rasilimali kwa misaada ya nje ya ziada kwa maendeleo yake, kwa kuzingatia uamuzi huo serikali itaimarisha mashirikiano yake na jumuiya za wahisani. Kwa hivyo haya maamuzi yametoka muda mrefu kwa nje tunaweza kupitia kwao lakini lakini kuzungumza tunazungumza moja kwa moja, lakini kwa misaada ya ndani hii moja kwa moja tunakopa wenyewe.

Mhe. Spika, hakuna uwiano wa maendeleo baina ya Pemba na Unguja baina ya Mkoa na Mkoa Mhe. Raishid Seif Suleiman kasema serikali ingechukua jitihada maalum kwa sababu kumeshakuwepo uwiano wa maendeleo baina ya visiwa vyetu viwili, hili tumekuwa tunalisema mwaka hadi mwaka na mambo yanaonekana, maeneo makubwa yaliyofanyiwa uwekezaji ni pamoja na Elimu, Afya, Kilimo, Barabara, Umeme, Maji safi n.k.

Miradi ya maendeleo kwa maeneo haya yote imewekezwa kwa visiwa vyote viwili isipokuwa tu kwa miradi inayohusu eneo maalum mfano uendelezaji wa kijiji cha millennium Micheweni, kigezo chengine cha muhimu kwa undelezaji ni idadi ya watu eneo na ukubwa tatizo linalotatuliwa kama vile barabara.

Mhe. Hijja Hassan Hijja alizungumzia suala zima la SUZA upande wa maabara kwamba wanafunzi wanakwenda bara kufanya *practical*, ufupi tu nataka kumwambia Mhe. Hija kwamba SUZA wamo katika jitihada za kuanzisha kitengo cha utafiti na kamati ya muda kwa ajili ya shughuli hiyo tayari imeshaanzishwa, hivyo kitengo kitakapoimarika na kufanya tafiti mbali mbali serikali itazitumia tafiti hizo, pamoja na hali hiyo serikali imekuwa ikiwatumia wataalam wa SUZA katika tafiti nyengine na masuala mengine ya ushauri.

Mhe. Spika, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar yaani SUZA unafadhiliwa na benki ya Kiarabu kwa maendeleo ya Afrika yaani BADEA pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, badea wamekubali kuchangia dola za kimarekani milioni 5.6 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechangia dola za kimarekani zipatazo 1.69 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kitengo cha ufundi, ujenzi wa kitengo cha sanaa na sayansi, ujenzi wa maktaba pamoja na ujenzi wa barabara ziliomo ndani ya Chuo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa sasa chuo hakina maabara kwa ajili ya kufanya tafiti mbali mbali yaani *research* hata hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika uwamu ya pili ya ujenzi wa Chuo hicho kina mpango wa kujenga jengo hilo kwa ajili ya kufanyia tafiti mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa ujenzi wa barabara Mhe. Hijja Hassan Hijja alitaka kujua matumizi ya shilingi milioni 450 na pia alikuwa na wasi wasi wa muda unaotumika kwa ujenzi wa barabara, barabara ya Kenya/Chambani maelezo mengi yametolewa na Mhe. Machano Othman Said na namshukuru sana kwa kuyatolea ufafanuzi kwa kina kabisa na nafikiri sihitaji tena kugusia upende huo, naamini Mhe. Hijja na waheshimiwa wengine hasa kwa upande wa zile barabara za Pemba Mhe. Machano amezungumza kwa ufasaha kabisa na tunamshukuru sana kwa ufuatiliaji wa karibu zaidi kwa masuala haya ya ujenzi wa barabara huko Pemba.

Mhe. Spika, marekebisho ya mashirika ya Serikali hilo nalo Mhe. Hijja alilliuliza Shirila la Meli na MV. Mapinduzi imeuzwa pesa zikowapi naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba ni kweli kwamba mashirika mbali mbali ya serikali likimo Shirika la Meli yapo hali mbaya kifedha na kiuendeshaji, kwa upande wa Shirika la Meli pia kuna tatizo la uchakavu wa meli zake na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji. Meli ya MV. Mapinduzi imeshakaa sana na serikali kama mmiliki pekee wa shirika hilo kushauriwa kuiuza tayari hatua za kuiuza zimekamilika na fedha hizo zipo hazina.

Mhe. Hijja Hassan Hijja alitaka kujua suala la deni la taifa serikali ichukue hatua za kulipa deni la muda mrefu la mchele unaodaiwa Thailand kweli tunakubali hii imekuwa ni kero sasa na kashfa kwa nchi, hii kampuni ya *Rice Company Limited* ndio inayotudai hasa hilo deni kongwe la mchele, deni hilo linatokana na ununuzi wa mchele uliofanywa na Shirika lililokuwa la Bizanje katika mwaka 1985 sote tunakumbuka wakati huo utaratibu wetu ulikuwa unakwenda je? Kwa kuwa Bizanje imefungwa kufuatia uregezaji wa masharti nchini Mahakama iliamua kulihamishia deni hilo kwa serikali, serikali kwa upande wake imechukua juhudi kubwa kulipatia ufumbuzi deni hilo zikiwemo za kufanya mazungumza na mdai na pia kutumia fursa ya ununuzi wa madeni yaliyojitokeza kupitia ufadhili wa benki ya dunia.

Kwa bahati mbaya mdai alikataa fursa zote zilizopendekezwa katika kulipatia ufumbuzi suala hilo la muda mrefu, serikali itafutilia fursa kama ipo ya kufanya tena mazungumza juu ya deni hilo kama sasa huyo mdai yupo tayari, ukweli ni kwamba malimbikizo ya riba yaliyokuwepo hayalipiki na hata kile chanzo chenyewe cha ile riba nayo nafikiri ilikua na matatizo, basi imepelekea ile riba kuwa kubwa zaidi. Kwa hivyo tunakiri na serikali kwa kweli tumeanza upya kutafuta juhudi za kuzungumza naye huyu anayetudai.

Mhe. Spika, mapato ya serikali badala ya kutegemea vianzio vilivyopo kulikuwa na haja ya kutafuta vianzio vipya vya mapato. Mhe. Salmin Awadh hili alilizungumza, Mhe. Hija na waheshimiwa wengine. Mhe. Salmin alisema kwamba uimarishaji wa maeneo huru ya uchumi haukupewa fedha za kutosha shilingi milioni mia moja tu.

Nataka kusema kwamba serikali kila aliyepata fursa hutafuta vianzio vipya vya mapato. Sehemu kubwa ikiwa ni yale mapato yanayotokana na kodi, hilo ndio suala la msingi. Wenzetu nchi za nje wengi sana wanaitumia kodi kama ni kianzio muhimu sana cha mapato nchini mwao. Mfumo wa kodi za serikali unategemea kodi za uingizaji za ulaji na zile zitokanazo na pato ama la kuajiriwa au faida.

Mhe. Spika, moja ya msingi muhimu wa kutoza kodi ni haja ya kuzingatia uwezo wa walipa kodi. Tusije kufanya kama ilivyozungumzwa jana, tukamkamua huyu anayelipa kodi mpaka tena yale maziwa hawezi kuyatoa ikawa baada ya kupata maziwa ikawa tunapata damu, sio lengo letu. Kwa hivyo haya mambo ni lazima tuyazingatie, tufanye uiyano ili tuone hiyo kodi tunaitoa wapi na kwa kiasi gani. Wananchi wetu wengi ni masikini hilo tunakubali na hivyo ni muhimu kuzingatia hali hiyo wakati wa kuibua vyanzo vya mapato na upeo wa kodi.

Mhe. Spika, ninachotaka kuelezea *observation* ndogo tu Baraza lako tukufu kwamba nimejaribu ku – *court* Bajeti ya Serikali kwa mwaka

2000/2001	Shilingi bilioni sabini na tano elfu, mia sita hamsini na tano.
2005/2006	Shilingi bilioni mia moja hamsini na saba elfu mia nne thamanini na nne.
2010/2011	Shilingi bilioni mia nne arubaini na nne mia sita thalathini na saba

Nataka tuone ile tofauti kutoka bilioni sabini na tano, ikenda bilioni mia moja hamsini na saba, sasa bilioni mia nne arubaini na nne. Pesa hizi tutazipata wapi? Sasa nataka ni *court* pia karafuu tulizokuwa tukiuza huko nyuma, nilikwenda kwenye mafaili na nashukuru sana wenzetu wa ZSTC, wamenipatia

takwimu za uzalishaji wa karafuu kuanzia mwaka 1964/1965 mpaka mwaka jana, takwimu zote *toneage* ya karafuu iliyouzwa nchi za nje na thamani yake. Sipendi kui-*court* yote itachukua muda mwingi. Lakini ninachotaka kusema ile *fluctuation* iliyopo ya uzazi wa karafuu na thamani iliyokuwa inauzwa nchi za nje na pesa iliyokuwa inapatikana.

Naomba nieleze pesa zilizokuwa zimepatikana kwa kuuza zao la karafuu mwaka wa juzi 2008/2009 ziliuzwa tani efu tatu mia tisa na moja. Fedha zilizopatikana ni shilingi bilioni kumi na moja, milioni mia tano ishirini na nane, mia sita kumi na tatu mia tisa hamsini na tatu.

Sasa shilingi bilioni kumi na moja ndio kwa mwaka mzima mzima 2008/2009. Sasa ninachotaka kusima jinsi bajeti yetu ilivyoongezeka na uwezo wetu kwa wakati huo basi tungepata matatizo makubwa kwenye uendeshaji wa serikali. Lakini sasa tizama pengo lilivyozibwa katika kodi zetu za ndani. Katika kodi, serikali katika kutafuta fedha na kutanua kutafuta vyanzo vyengine vya serikali, basi serikali imejitahidi kutafuta vyanzo vyengine.

Kwa ufupi mwezi Mei mwaka huu ZRB tu wamekusanya shilingi bilioni saba, mwezi mmoja tu, ambapo mauzo ya karafuu kwa mwaka mzima mwaka juzi tumepata bilioni kumi na moja. Naonesha ile umuhimu wa serikali ilivyotoa fursa kwa *ivestment* kufungua mahoteli, kufungua vianzio vyengine vya mapato ili kuweza kuiendesha serikali na mapato mengine. Inaonesha vipi tumekuwa na nimeonesha vipi bajeti ya serikali imeweza kukua. Hii nasisitiza kwamba bado tunahitaji vianzio vipiya vya mapato na kudumisha mapato yetu tuliyonayo na tuweze kuyakusanya vizuri.

Lakini pia kwenye karafuu hatudharau bado makusanyo yapo na naomba sana tuwashajihishe wakulima wetu wa karafuu, wasafishe mashamba yao tusingoje mpaka wakati wa uzazi tu wanakwenda wanasafisha, tuyasafishe wakati wote, wakati wa uzazi pale tunazichuma vizuri tunauza. Nimetoa *comparison* hizi makusudi kuonesha tulitoka wapi tupo wapi na tunaelekea wapi kimapato. Haja yetu ingekuwa bado tupo kwenye karafuu tu, tungekuwa wapi leo jamani.

Nakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi tuna *role* kubwa kuhimiza ukusanyaji wa kodi ni muhimu sana na umetusaidia. Hili ni suala la msingi nchi zote, ao wahisani wanaokuja wakati mwengine tunaona haya, wanatusimbulia wanasema hizi pesa za walipa kodi wetu mzitumie vizuri kwa hivyo na sisi hebu tuhimize walipa kodi wetu na wao wachangie tusaidiane na huu uzalishaji wa karafuu. Mhe. Spika, nilihisi hili nalo kidogo nilitolee ufafanuzi au maelezo ili litusaidie katika kuwashajihisha wakulima wetu wazalishe zaidi.

Mhe. Spika, suala la CDF, lilizungumzwa kwa urefu, Mhe. Fatma, Mhe. Ali Abdalla, Mhe. Abubakar, Mhe. Ame Mati, Mhe. Thuwaybah, Mhe. Suleiman Hemed, nafikiri kama nilivyoeleza hapo awali kwamba juhudi tunaziendeleza basi sitaki tena kurejea.

Katika Programu ya Mageuzi ya Matumizi ya Umma ni hekaya ya Abunuwasi imechukua muda mrefu. Mhe. Haji Faki Shaali, msamiati mzuri umeutumia. Nataka kusema kwamba ingawa Programu ya Mageuzi ya Matumizi ya Umma imechelewa, hata hivyo napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa programu hiyo imekamilika na utekelezaji umeshaanza, tulipata msaada wa Benki ya Dunia kidogo na tunakwenda nao na *Alhamdulillah* tunakwenda nao ilibidi wa-*review* mambo yaliyoopo halafu washauri na mambo kidogo yalingane na hali yetu ya kisiasa na tunavyokwenda. Kwa hivyo ni mambo mengi sana kuzingatiwa. Sasa hivi tunakwenda sambamba na wenzetu wa Tanzania Bara katika programu hii tunakwenda nao pamoja.

Mhe. Spika, Mhe. Mazrui alisema kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi, jengo ambalo limeanguka Pemba nako kunaashiria kuwepo kwa ubadhilifu. Tunataka kusema kwamba ah! Tunasema ile ni ajali Mhe. Mazrui, usitafute mchawi, labda mchawi tuseme ni mjenzi mwenyewe na *contracture*, naona waheshimiwa wengi wameanza kuliulizia hili. Ukweli wala halijaanguka, maana ukisema limeanguka ni kwamba lote limeporomoka aaa. Ni sehemu fulani tu imeanguka na ile zaidi zile nguzo nafikiri. Ali-*under value* na pale pana maji zile nguzo *strength* yake ni ndogo kwa hivyo ile kazi niseme pale kidogo aliteleza. Hili tutalitolea taarifa kwa urefu itakapokuja bajeti yetu ya Wizara ya Fedha. *In such* halijaanguka limemong'onyoka kidogo lakini kuna wasi wasi huko mbele hali itakuwaje. Hili mwenyewe *consultant* na mjenzi tunawaachia, sisi taratibu zote tumezifata kumtafuta *contracture* na ujenzi wake ni utalamu wake tu yeye mwenyewe mjenzi. Tukuchukulie ni ajali tu.

Nimependa ile *point* ambayo Mhe. Waziri Kivuli asubuhi alisema, akawaorodhesha wakandarasi, kuwapima uwezo wao na hali yao kwa ujumla. Hili tutalizingatia kwa serikali nzima huko mbele.

Pia alizungumzia takwimu za ajira zinazogongona na kuwa ni tofauti na takwimu za wafanyakazi inahitaji maelezo, hili nafikiri tulilitolea maelezo. Serikali imeendelea kutumia takwimu mbali mbali katika vigezo vyake. Mfano utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ya mwaka 2004/2005 aliutaja Mhe. Ali Abdalla ndio uliotumika kuonesha Wilaya zilizo na umasikini zaidi na hivyo serikali kuongeza nguvu katika Wilaya hizo.
Mgao wa rasilimali kisekta, Mhe. Juma Duni na yeye alizungumzia sana kwenye suala hili na akasema kwamba sekta ya utalii haidhuru kuwa ni *contributor* mkubwa lakini iko chini katika kupewa mgao wake. Nataka

kusema kwamba mgao wa fedha kwa sekta ya utalii uangaliwe na maendeleo ya mgao kwa sekta nyengine hasa za miundo mbinu. Aidha pia tuangalie katika utoaji wa huduma kwa sekta ya umma na sekta binafsi na kwamba kwa ujumla huduma ya utalii inatolewa zaidi na sekta binafsi na serikali huweka mazingira mazuri tu ili sekta hiyo iweze kuhuika.

Mtakumbuka kuwa wakati serikali ilipoanza kuvutia wawekezaji karibu miundombinu mingi haikuwa ya kuridhisha na hivyo serikali ilipata wakati mgumu kuvutia wawekezaji hususan katika sekta ya utalii. Nakumbuka zamani tunataka kwenda Hoteli ya Karafuu Michamvi kule tulikuwaje au Hoteli za Kiwengwa maana unajiuliza mara mbili mbili, lakini leo mgongo wa ngisi unakwenda na unarudi si mara moja si mara mbili. Kwa hivyo nafikiri hayo ndio *promotion* na ilikuwa umeme ulikuwa haupo, maji yalikuwa hayapo. Kwa hivyo sasa hivi miundo mbinu hiyo *Alhamdulillah* tumeiwezesha na sekta ya utalii imekaa vizuri. Leo Kiwengwa kama alivyosema Mhe. Mati unaamua tu barabara gani utumie kuja mjini, unataka ya Kinyasini, unataka ya Kupitia kule Kiwengwa kwenyewe au unataka kupitia ya kati unaamua ipi uitumie mwenyewe.

Mhe. Spika, kwa hivyo serikali inatumia fedha nyingi kuweka miundo mbinu ya uhakika ambayo inanufaisha moja kwa moja sekta ya utalii. Miundo mbinu hiyo ni ukarabati na uwekaji huduma wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar .

Ujenzi wa Bandari, barabara, umeme, mawasiliano ya simu, maji na kadhalika. Hivi sasa maeneo mengi ya utalii ya Kaskazini Mashariki, Mashariki na Kusini, miundo mbinu hiyo imeimarika kama nilivyosema. Aidha fedha zinazowekwa kwa sekta ya utalii hutumika zaidi katika kukuza na kutangaza Zanzibar ambazo kazi hii pia inafanywa na sekta binafsi zaidi kwa kutangaza bidhaa hizo. Hivyo fedha zinazopelekwa katika maeneo ya miundu mbinu, elimu, kilimo, maji safi na hata afya zinanufaisha moja kwa moja sekta ya utalii.

Mhe. Ali Abdalla alishauri kwamba mradi wa MCC wa umeme upunguzwe na fidia kwa wananchi iangaliwe ili Mwenye Kioski asilipe sawa na mwenye nyumba. Ushauri wake tunaukubali ni kabisa na labda kwa bahati mbaya kama ilifanywa hivyo sio lengo, hilo ni bahati mbaya basi tutakaa na hao waliofanya kazi hiyo kuweza kurekebisha hiyo hali.

Ukweli ni kwamba ratiba ya ukamilisha mradi wa MCC inaonesha kuwa utakamilika mwisho mwa maka 2012. Hata hivyo katika matayarisho ya utekelezaji wa mradi wasimamizi wa mradi wa MCC nchini yaani MCAT wamekaa na mkandarasi aliyeshinda zabuni ya utekelezaji na kukubaliana

kuwa mkandarasi ataandaa na kuwasilisha mpango wa utekelezaji ambao ndio utakaotoa muda hasa wa kukamilisha mradi huo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la fidia mradi huu kwa kushirikiana na serikali umechukua tahadhari zote kuona kwamba fidia stahiki inatolewa kwa wote wale ambao kuwa wataathirika na utekelezaji wa mradi huu. Kwa upande wa majengo wametumika wakadiriaji kutoka wizara inayohusika na ardhi na kwa mazao ukadiriaji kutoka wizara inayohusika yaani Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo kila *field* tumechukua yule muhusika mwenyewe akafanye hayo makadirio. Kwa hivyo tutajitahidi kuwa waadilifu kuona kwamba mambo yanakwenda kama ilivyopangwa na tusimnyime mtu haki yake.

Vigezo vilivyotumika katika fidia ya majengo ni pamoja na ukubwa wa jengo namna jengo lilivyojengwa katika umaliziaji, pahala jengo lilipo. Iwapo jengo kama linahusisha biashara kama vile mlango wa duka. Zaidi ya haya pia fidia itahusisha pia posho la usafiri, usumbufu na malazi wakati wa kuhama. Zoezi la ukadiriaji wa fidia pia limehusisha waathirika na kimsigni wote wameridhika.

Mhe. Spika, bajeti iliyopita ilipewa jina la bajeti ya miundo mbinu ya kilimo na utalii lakini haikutekelezwa. Mfano barabara ya Wambaa ambayo haipitiki, barabara ya Kusini Pemba chini ya Ufadhili wa Norway hazikupaswa kupewa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Mhe. Mula alizungumzia hili.

Nataka kumwambia kwamba miundombinu ya kuimarisha Kilimo na Utalii, mkazo uliwekwa katika kueneza mtandao wa barabara hususan za vijijini, Viwanja vya Ndege nishati ya umeme na kadhalika. Kuhusu matengenezo ya barabara ya Wambaa nafikiri Mhe. Machano ameelezea kwa ufasaha na ameelezea mpango mzima uliopo hasa kwenye barabara yake hii kwamba itashughulikiwa ipasavyo.

Uchaguzi wa miradi ya TASAF izingatie ile itakayodumu muda mrefu Mhe. Mula naye alizungumzia suala hili. Tunasema kwamba ushauri tumeupokea na tutautekeleza. Mhe. Tafana, Mhe. Zakiya, Mhe. Asaa walizungumzia suala zima la Tariff za TANESCO na maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayakutekelezwa juu ya ongezeko la Tariff hayajazingatiwa.

Nataka kusema kwamba ni kweli nchi yetu inahitaji chanzo mbadala cha kuaminika cha umeme wa gharama nafuu. Serikali inatambua umuhimu wa suala hili. Hata hivyo uwekezaji wa aina hiyo unahitaji fedha nyingi ambazo ni vigumu kuweza kukidhiwa kwa mapato ya ndani. Mkazo wa sasa ni kuanza njia itakayosaidia kupatikana kwa umeme huo kwa haraka sababu ambayo kwa sasa ni kuweka njia nyengine ya chini ya bahari kutoka Tanzania Bara. Serikali

itaendelea kushughulikia utafutaji wa chanzo mbadala cha umeme. Ushauri wetu waheshimiwa tumeusikia na tutaufanyia kazi.

Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Suleiman Khelef, walizungumzia suala zima la kupungua kwa mfumko wa bei, kwamba haulingani na hali halisi, bei za bidhaa bado zipo juu. Mhe. Spika, nataka kusema kwamba kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2009 imepungua hadi kufikia 8.9% ikilinganisha na kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2008. Sababu zilizotajwa katika kifungu 54 ni sababu zizopelekea kupungua kwa kasi hiyo kwa mwaka 2009 na sio kwa mwaka 2010.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010 athari za kuongezeka kwa bei ya mafuta na chakula zitakuja kuonekana katika mfumko wa bei kwa mwaka 2011. Matarajio ya mfumko wa bei kwa mwaka 2010 yanaonesha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma kwa wastani wa 7.8% hivyo viashiria vya uchumi vinatabiri kuwa bei za bidhaa na huduma zitapanga ingawa si kwa kasi kubwa zaidi.

Mhe. Muhunzi na Mhe. Suleiman Moh'd Khamis, waliulizia suala zima kwamba kuna haja ya kuangalia mfumo wa bajeti badala ya utarabu wa sasa kuangalia nyongeza. Kimahesabu inaonekana inalingana na wenzetu wa nchi za jirani. Asilimia ya mshahara kwa pato la taifa kwa Zanzibar ni 9% wakati Tanzania Bara na 17% kwa nini bado tupo chini?

Mhe. Spika, mfumo wa bajeti unaweza kufanyiwa mapitio kila baada ya muda lakini si kila wakati. Kiwango cha mshahara kwa asilimia 17 ya pato la taifa aliotaja Mhe. Muhunzi inamaanisha kwamba takriban fedha zote zinazokusanywa na SMT ambazo ni asilimia 18 ya pato la taifa zinatumika kulipia mishahara. Hii ina maana kuwa asilimia moja tu ya pato la taifa ndilo linalotumika kwa shughuli za maendeleo na kazi kawaida.
Ukweli wa taarifa hii unatia wasi wasi na vigumu kidogo kufahamu, inabidi tuufanyie kazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, Mhe. Thuwaybah alizungumzia suala la mizani ya biashara na kupungua uhaulishaji kwenda Bara na nakisi maana yake nini?

Mhe. Thuwaybah tunakushukuru na naomba kukujulisha tu kwamba nakisi katika urari wa biashara inapotokea kuwa thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje kuwa kubwa kulinganisha thamani ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Tarakimu inayopatikana ndio nakisi. Hali hiyo kwa Zanzibar inasababishwa na uwezo mdogo wa uzalishaji wa ndani, hali ambayo inapelekea kuagiza bidhaa nyingi muhimu kutoka nchi za nje.
Mhe. Thuwaybah pia aliulizia suala la kauli mbiu, tulitegemea kutolewa maelezo juu ya mafanikio ya kauli mbiu ya bajeti ya mwaka jana ana wasi wasi

kuwa fedha zote zinazokusanywa zitaelekezwa kwenye chaguzi na kura za maoni kwa mujibu wa kauli mbiu yetu ya mwaka huu.

Mhe. Spika, ukweli kwamba hakuna ulazima wa kuweka kwa kauli mbiu lakini ni muhimu katika kuonesha msisitizo wa bajeti. Aidha kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa kauli mbiu hiyo yameelezwa kwa kina katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 38 mpaka 42 na katika kitabu cha kwanza katika utekelezaji wa *cluster* ya kwanza kuanzia ukurasa wa 45 mpaka 80. Bajeti imetayarishwa kwa kuzingatia umuhimu wa uchumi, maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na demokrasia.

Mhe. Spika, naomba sana waheshimiwa hata sekta nyengine zinazokuja wajitahidi sana kupitia vitabu viwili vya mwanzo kabla ya hii bajeti ya serikali au kabla ya hizo bajeti za sekta. Kwa sababu hizi ni *summary* ya wizara. Hii hatukuandaa Wizara ya Fedha *in such*, tumeandaa na washiriki wenyewe wa Wizara kwa hivyo naomba sana sana waheshimiwa itawasaidia sana ukivisoma vitabu viwili hivi kabla ya kuigusia hiyo sekta yenyewe. kwa sababu hii ni *review*. Malengo yote yale ya mwaka jana na *performance* yote vile ilivyokwenda basi tumeyaweka humu.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa Mhe. Muhiddin aliuliza bakaa ya mafao ya wastaafu italipwa lini. Mhe. Muhiddin naomba kukwambiwa kwamba pale tulipotoa *figure* zetu zile tulikuwa nyuma lakini *to date* bakaa hiyo imeshalipwa tokea mwezi wa April mwaka 2010. Hiyo bakaa tunayoitaja ya wastaafu kwa hivyo wanaotarajiwa kustaafu wasiwe na wasi wasi, mambo yao yapo. Waheshimiwa wajumbe nyinyi sio wastaafu lakini mambo yenu pia yapo.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna michango ya leo hasa Mhe. Fatma aliuliza mambo mengi kidogo ya *technical* lakini nataka kumwambia tu kwamba mambo yake mengi pengine nimeyajibu hapa na pale lakini kuhusu zile *balance of payments* au zile pesa zilizotolewa na IMF zile shilingi mia tatu milioni kwa mwaka 2010 kwa ajili ya kusaidia urari wa malipo. Fedha hizo zilitolewa na Shirika la Fedha la Dunia, hata hivyo fedha hizo hazikugaiwa kwa serikali yaani yazikupelekwa kwa SMT wala SMZ zilipelekwa Benki kuu kwa madhumuni ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni. akiba hii ilisaidia kulinda thamani ya shilingi kutokana na kupungua kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na msuko suko wa fedha duniani.

Kuhusu suala la utekelezaji wa Mkuza nafikiri tumelieleza vizuri na kama nilivyosema maelezo mengi yamo kwenye kitabu.

Kuhusu mapato ya makadirio ya Wizara kushuka makadirio ya mapato ya Mawizara yanaonekana kushuka katika mwaka wa fedha 2010/2011. Hali hii

inatokana na baadhi ya idara za serikali kufanywa mamlaka. Hivyo makusanyo yao yanatakiwa kutumwa moja kwa moja na taasisi hizo bila ya kuingizwa katika mfuko mkuu wa serikali. Tasisi hizo ni Mamlaka ya Uvuvi na Bahari Kuu pamoja na Shirika la Magazeti ya Serikali hiyo ndio sababu kubwa kwa kushuka kwa mapato ya mawizara na serikali.

Mhe. Spika, nimejitahidi sana kuzijibu hoja za waheshimiwa wajumbe kadiri ya uwezo wetu. Niwashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Wizara nyengine kwa ujumla kwa kurahisisha majibu yangu. Nataka kusema sisi tuchukulie suala la bajeti ya serikali na suala la uchumi wa nchi tulichukulie kwamba linatuhusu sote Waheshimiwa Wajumbe. Tuna jukumu kubwa la kuwashajihisha au la kushajihisha uzalishaji, kuhimiza usimamizi wa ukusanyaji kodi. Hayo yote yanakuja kwa upendo na umoja kati yetu na tuone kwamba hili sio langu, naomba tulione kwamba hili ni letu. Mhe. Saidi ukiwa Gando pale tusaidie, ukiona chochote tujulishane ili hili letu lende.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumuomba sana Mhe. Ame Mati Wadi, mlango wangu wa Afisini uko Ikulu, hajaja na wakati wowote akija nitampikia chai na masalo lakini hajaja, asiseme kaja.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Sasa kazi iliyobaki ni kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio na Mapato kwa ajili ya Bajeti ya Serikali wanyenye mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana. Ratiba yetu ni kwamba Afisi ya Waziri Kiongozi tuanze kesho. Nimepewa taarifa kwamba vitabu tayari vimetolewa kwa wajumbe, wale ambao hawajavipata basi wahakikishe kwamba wanavipata ili wakaanze kujisomea na kesho iwe rahisi kuifanya kazi yetu.

KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi (AWK): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri Kiongozi kwa kuwa shughuli zetu tulizojipangia leo zimemalizika, kwa kwa kuwa jioni tutakuwa hatukupata shughuli nyengine kuendelea. Naomba

uliakhirishe Baraza hadi kesho siku ya Alhamis saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Maombi yanakubaliwa, waheshimiwa wajumbe tunajitayarisha kwa ajili ya shughuli za kesho kwa hivyo tukahakikishe kwamba tunafanya shughuli zetu vizuri. Nakumbuka kumbe tulirekebisha kanuni. Maana kaomba kumbe ilikuwa ni kazi ya Spika, kwa kuwa shughuli tumearifiwa kwa leo hakuna nyengine basi tuahirishe shughuli zetu moja kwa moja ili tuje kesho.

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuahirisha Kikao hichi hadi tarehe 17 siku ya Alhamis Saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 6:30 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 17/06/2010)
Saa 3.00 asubuhi)